SportPesa
TZS. 761,374,640
NI YA KWAKO WIKI HII,
BETI LEO UWE MILIONEA
SPORTPESA.CO.TZ PIGA *150*87#



**Korti** yalitupa ombi la Sabaya dhidi ya shahidi

UKURASA 3



Mbappe aeleza kuumia kutojiunga Real Madrid

UKURASA 21


# Nipashe

Jumanne Desemba 7, 2021 Tanzania 1,000/- Kenya 100/-

MWANGA WA JAMII

ISSN 0856 • Na. 0580787

www.ippmedia.com

www.twitter.com/nipashetz
www.facebook.com/nipashetz
www.instagram.com/theguardian_newspaper
LIKE & FOLLOW US




# Waziri aibua uozo unaoua mashirika

• **Aanika** namna bodi zinavyochangia... *Endelea ukurasa 2*



Rais Samia Suluhu Hassan akikata utepe kuzindua rasmi awamu ya kwanza ya kiwanda cha vifaa vya umeme cha Elsewedy Electric East Africa Ltd kilichoko Kisarawe II Kigamboni jijini Dar es Salaam jana. **PICHA: IKULU**

## Ajinyonga hadi kufa kutotajwa misa ya shukrani

UKURASA 3



Scan Hapa
Fungua App ya QR Code Reader kisha scan kupakua APP yetu



Ofisa Mkuu wa Fedha wa Benki ya CRDB, Fredrick Nshekanabo, akipokea tuzo ya mshindi wa jumla kwa Uwasilishaji Bora wa Taarifa za Fedha nchini kwa viwango vya kimataifa, kutoka kwa Mhasibu Mkuu wa Serikali, Leonard Mkude (kushoto), zilizotolewa na Bodi ya Taifa ya Wahasibu na Wakaguzi wa Hesabu Tanzania (NBAA), katika hafla iliyofanyika kituo cha mikutano cha NBAA, Bunju Dar es Salaam, mwishoni mwa wiki. Kulia ni Mtaalamu wa Uendeshaji wa Fedha wa Benki ya CRDB, Neema Maganja. **NA MPIGAPICHA WETU**

## Samia ataka wazalendo kuwekeza viwanda vya ndani

UKURASA 2

**MICHEZO** SAMIA TAIFA CUP KUNGURUMA DAR IJUMAA UK.20 | MAONI, KATUNI UK.6

# Waziri Mbarawa aibua uozo unaoua mashirika

**Na Gwamaka Alipipi**

WAZIRI wa Ujenzi na Uchukuzi, Prof. Makame Mbarawa, amefichua uozo unaochangia mashirika mengi ya umma kufeli katika utendaji.

Amefichua sababu kubwa inayochangia ni bodi za mashirika hayo kutanguliza maslahi binafsi na kwamba ndio maana bodi nyingi zinavunjwa.

Kwamba zinavunjwa kutokana na kushindwa kusimamia ununuzi, maslahi binafsi pamoja na kuendekeza urafiki.

Amesema bodi nyingi zilishindwa kutimiza majukumu waliyopewa kutokana na baadhi ya maofisa watendaji wakuu wa mashirika kuwashika wajumbe wa bodi, hali inayosababisha kila jambo wanalopelekewa kulipitisha pasipo kuhoji.

Aliyasema hayo jana jijini Dar es Salaam wakati akizundua Bodi ya Shirika la Ndege Tanzania (ATCL), huku akiwatahadharisha wajumbe hao kuwa makini katika utendaji kazi wao, vinginevyo hawatadumu muda mrefu.

Alisema wajumbe wa bodi wengi wanakuwa na 'personal interest' (maslahi binafsi) hali inayowasababishia kujisahau kutimiza majukumu waliyopewa.

"Nikiona mtu anazembea namnyofoa namweka mwingine, hivyo hivyo hadi mambo yatakapokaa sawa. Wajumbe wengi wa bodi wanashindwa kusimamia majukumu yao, wanakuwa sehemu ya uongozi wa shirika," alisema Prof. Mbarawa na kuongeza:

"Mkiacha urafiki na mtu mtafanikiwa. Nendeni mkalisimamie shirika, Ma-C.E.O (maofisa watendaji wakuu) wanatabia ya kuwashika wajumbe wa bodi, muwe na tabia ya kuuliza kila kitu siyo kila mnacholetewa mnakipitisha."

Prof. Mbarawa alisema watu wengi wanafurahi wanapoteuliwa kuwa wajumbe katika bodi kwa sababu wanafahamu ni sehemu ya kukaa na kupata pesa.

"Bodi ni sehemu ya kumsaidia waziri na taasisi kutimiza malengo, lakini wengi wanakuwa na maslahi binafsi. Bodi ya ATCL mnakazi kubwa, manunuzi ni makubwa sana ATCL nendeni mkalisimamie hilo, jengeni tabia ya kuuliza, tukifanya hivyo kila mtu atakuwa salama, familia zenu zitakuwa salama."

Kadhalika, Prof. Mbarawa aliwataka wajumbe wa bodi hiyo kuhakikisha ATCL inakuwa pamoja na kuzisimamia ndege zijiendesha kwa faida.


Aliwataka wajumbe hao kuhakikisha ATCL inakwenda kwenye soko la ushindani pamoja na kutoa huduma bora kwa wateja.

"Soko la ATCL bado halikajaa vizuri, hivyo ni kazi yenu kuisukuma menejimenti. Baada ya miaka miwili tutakuwa na ndege zaidi ya 17 ni jukumu lenu kuzisimamia ndege hizo," alisema Prof. Mbarawa.

Naye Mwenyekiti wa Bodi ya ATCL, Profesa Neema Mori, alisema: "Tutatimiza matakwa na malengo ya wateja wetu, pia tutahakikisha ATCL inakwenda katika malengo yaliyopangwa. ATCL kuwa shirika la mfano, bora, pamoja na kutoa huduma zinazokidhi viwango."

Mkurugenzi Mkuu wa ATCL, Ladislaus Matindi, alisema kwa sasa shirika hilo linaingia katika ushindani wa kibiashara na mashirika mengine ya ndege.

Alisema kwa sasa imeboresha huduma za usafiri na imejipanga kufika katika miji mingi zaidi barani Afrika na nje ya Afrika.



Rais Samia Suluhu Hassan, akimwapisha Prof. Adelardus Kilangi kuwa Balozi wa Tanzania nchini Brazil, Ikulu jijini Dar es Salaam jana. **PICHA: IKULU**

## ...Aahidi kushughulikia tozo daraja Kigamboni

**Na Jenifer Gilla**

RAIS Samia Suluhu Hassan ameahidi kuifanyia kazi kero ya tozo wanayokatwa wakazi wa Kigamboni na wengine wanaopita katika daraja jipya la kisasa liliko eneo hilo.

Alitoa ahadi hiyo aliposimama kusalimia wananchi wa Kibada, wilayani Kigamboni, akiwa njiani kuelekea katika Uzinduzi wa Kiwanda cha Elswedy Electrical East Africa Limited jijini Dar es Salaam.

Alikuwa akijibu malalamiko ya Mbunge wa Kigamboni, Faustine Ndugulile, alipotoa kero tozo ya Sh. 5,000 wanazotozwa wakazi wa eneo hilo wanapopita katika daraja la Kigamboni.

"Daladala moja ikivuka pale inakatwa Sh. 5,000, ikipiga tripu 10 za kwenda na kurudi sawa na mara 20 hiyo ni laki moja anaiacha darajani, hapo hajakata mafuta, wala pesa ya tajiri, wala hela yake," alisema.

"Lakini kwenye suala la tozo mheshimiwa mbunge naomba nilichukue na ninaahidi kulifanyia kazi," alijibu Rais Samia.

Mbunge huyo pia aliwasilisha kero ya miundombinu mibovu ya barabara inayowakabili wananchi wa eneo hilo. Alisema ni asilimia 37 tu ya barabara za TANROADS Kigamboni zimepigwa lami, katika asilimia 100 ya barabara ambazo hazijapigwa lami katika Mkoa wa Dar es Salaam, asilimia 50 zinatoka Kigamboni.

Rais Samia alijibu kuwa serikali imeandaa Sh. bilioni 21 kwa ajili ya kushughulikia kero hiyo katika jimbo hilo na maeneo mengine ya Dar es Salaam.

# Samia ataka wazalendo uwekezaji viwanda ndani

**Na Jenifer Gilla**

RAIS Samia Suluhu Hassan amewataka wawekezaji wa ndani kuchangamkia fursa ya uwekezaji katika viwanda, ikiwa ni njia mojawapo ya kujikwamua kiuchumi kwa kuepuka utegemezi wa kuagiza bidhaa kutoka nje ya nchi.

Aliyasema hayo jana wakati akizindua kiwanda cha nyaya za transfoma na umeme cha El Sewedy kilichoko Kisarawe, Wilaya ya Kigamboni mkoani Dar es Salaam kilichojengwa na wawekezaji kutoka Misri.

"Tunaposherehekea siku hii muhimu na adhimu (miaka 60 ya Uhuru) ni lazima kutafakari maazimio yetu tuliojiwekea mwaka 1961 ya kujikomboa kiuchumi, kwa kuondoa utegemezi wa kuagiza bidhaa kutoka nje na kuongeza uzalishaji wa ndani," alisema.

Rais alisema kiwanda hicho kitazalisha bidhaa za teknolojia ya hali ya juu kwa kuzalisha tani 15,000 za nyaya za umeme, transfoma 1,500 na mita za 100,000 za umeme kwa mwaka.

"Nusu ya bidhaa hizi zitauzwa masoko ya nje na kuongeza ujazo wa pesa za kigeni, aidha kinachobaki kitatumika nchini na kuondoa utegemezi wa bidhaa za nje," aliongeza.

**VIWANDA KIGAMBONI**

Alisema pia Wilaya ya Kigamboni itakuwa eneo maalum la uwekezaji ambapo wawekezaji watalelekezwa kujenga viwanda vyao huko.

"Kwa hiyo Kigamboni sasa linakuwa eneo maalum ambapo wawekezaji watalelekezwa kuja kama mlivyosikia, tutakuwa na industrial city (mji wa viwanda) ambao utakuwa na uwekezaji mwingi ndani yake."

Aliahidi kushughulikia changamoto za maji, umeme na barabara zinazoikabili wilaya hiyo ili kunyoosha njia ya uwekezaji.

"Natambua katika eneo hili kuna changamoto ya barabara... na kwa sababu tunafungua Kigamboni kuwa eneo la viwanda pia, kipaumbele cha kwanza kitatolewa kuhakikisha maeneo yote yana umeme, yana maji na barabara za lami, " alisema.

"Ndugu zangu niwasihi sasa wote wanaonisaidia, tuachane na mtindo wa kazi tuliozoea, kama tulikuwa tumezoea uwekezaji wa Dola milioni nane, milioni tisa, sasa wanaokuja ni wa madola mengi mengi," alisema Rais Samia.

Alisema pia ziangaliwe fursa chanya zinazopatikana katika janga la Covid-19 kufunguka kiuchumi.

"Maradhi haya ya Covid-19 upande mwingine ni mabaya upande mwingine yametoa fursa kwa Bara la Afrika kufunguka kiuchumi, mapinduzi ya nne ya viwanda yamefungua Bara la Afrika, lakini maradhi haya yamefungua zaidi ...kwa kudra za Mwenyezi Mungu Dar es Salaam tumewekwa pazuri...kama lango la kuingilia Afrika yote," alifafanua.

Aliwashukuru wageni 111 kutoka Misri wakiwamo wawekezaji wakubwa 40 waliokuja kuangalia fursa za uwekezaji nchini na kumsisitiza Waziri wa Uwekezaji, Godfrey Mwambe, kuwaonyesha fursa.

Mkurugenzi wa Kiwanda hicho Afrika Mashariki, Ibrahim Kamal, alisema nyaya za umeme na transfoma zinazotengezwa kwa kiwango cha juu, kati na chini, kitanufaisha wakazi wa vijini na vijijini na kinatarajia kutoa fursa ya ujuzi wa masuala ya umeme kwa Watanzania na ajira 500.

## HABARI KITAIFA

# Korti yalitupa ombi la Sabaya dhidi ya shahidi

**Na Allan,** ARUSHA



MAHAKAMA ya Hakimu Mkazi Mkoa wa Arusha, imetupilia mbali ombi la mawakili wa upande wa utetezi, wakiiomba mahakama hiyo, kuruhusu kukamatwa kwa mfanyabiashara Francis Mroso, wakidai kwamba alitoa rushwa ya Sh. milioni 90.

Mroso, ambaye ni shahidi wa 10 wa Jamhuri katika kesi ya uhujumu uchumi namba 27, inayomkabili aliyekuwa Mkuu wa Wilaya ya Hai mkoani Kilimanjaro, Lengai Ole Sabaya na wenzake sita, wakati akitoa ushahidi mahakamani huko, alidai kwamba alilazimishwa kutoa rushwa ya Sh. milioni 90.

Katika kesi hiyo, mbali na Sabaya washtakiwa wengine mbali na Sabaya katika shauri hilo ni Silvester Nyengu(26), Enock Togolani(41), Watson Mwahomange(27), John Odemba, Jackson Macha(29) na Nathan Msuya(31).

Akitoa uamuzi mdogo, Hakimu wa mahakama hiyo, Patricia Kisinda, alisema mahakama imetupilia mbali ombi hilo, kwa kuzingatia vifungu vya sheria ikiwamo sheria namba 141 ya mwenendo wa ushahidi kifungu cha 52(1) ya TAKUKURU.

Alisema kwa pamoja vifungu hivyo vya sheria haviruhusu shahidi kushtakiwa hata kama anatuhumiwa yeye mwenyewe.

Kadhalika alisema kifungu namba 17 cha sheria ya mwenendo wa makosa ya jinai, kinaeleza wazi kuwa shahidi huyo, alitoa ushahidi chini ya kiapo na alieleza mahakama ukweli juu ya kutoa rushwa ya Sh.milioni 90, hivyo shahidi analindwa kwa mujibu wa sheria.

Hakimu Kisinda, alisema shahidi akiwa chini ya kiapo alizungumza ukweli kwa ametoa rushwa hivyo anapaswa kulindwa kutokana na vifungu vya sheria tajwa ambavyo vimekidhi matakwa ya kisheria na mahakama haiwezi kutoa amri ya shahidi kukamatwa na kushtakiwa kama alitoa rushwa hivyo ameitupilia mbali hoja zilizowasilishwa na mawakili wa utetezi.

"Mahakama imezingatia kifungu cha sheria ya mwenendo wa ushahidi na maombi ya wakili wa utetezi hayakukidhi matakwa ya kisheria kutokana na hilo mahakama imetupilia mbali ombi hilo, kwa kuwa limewasilishwa kinyume wa sheria ya ushahidi,"alisema Hakimu Kisinda.

Baada ya kutoa uamuzi huo, kesi hiyo itaendelea tena leo, kwa shahidi wa 11 wa Jamhuri kuanza kutoa ushahidi.

Desemba Mosi mwaka huu, Wakili wa Utetezi, Fridolin Bwemelo, aliwasilisha ombi la kukamatwa kwa shahidi huyo, Francis Mroso, akidai kwamba alitoa rushwa ya Sh. milioni 90 na yupo uraiani na aliowapatia rushwa ni washtakiwa kwenye kesi hiyo.

Alidai kwa mujibu wa Sheria ya Kupambana na Rushwa Kifungu cha 15(1B), kimeeleza wazi hatua za kuchukuliwa kwa mtu atakayetoa na kupokea rushwa na hakuna kifungu kinachoeleza kuna rushwa ya kulazimishwa kutoa.

Alieleza kwa mujibu wa kifungu hicho cha sheria hakuna sehemu kimezungumzia suala la kutoa rushwa kwa kulazimishwa kwa kuwa mtoaji na mpokeaji wa rushwa watakuwa wametenda kosa.

Vilevile aliomba kupata tafsiri ya mahakama kwa kuwa kesi ilifunguliwa na TAKUKURU, na ilitakiwa kuendeshwa na mawakili wake, badala ya mawakili wa serikali kama ilivyofanyika.

Victoria FINANCE

Victoria Finance Plc
5th Floor, Sky Tower Building-Kijitonyama
New Bagamoyo Road
P.O. Box 12102, Dar es Salaam - Tanzania
Telephone +255 22 277 4577
Fax: +255 22 277 4559
Email: info@victoriafinance.co.tz
Website: www.victoriafinance.co.tz

**TANGAZO LA MINADA YA HADHARA**

VICTORIA FINANCE PLC INAPENDA KUUTANGAZIA UMMA WA WATANZANIA YA KWAMBA KWA IDHINI ITAKAYOTOA KWA KAMPUNI TOFAUTI ZA UDALALI INATARAJIA KUUZA KWA MNADA WA HADHARA DHAMANA ZA WADAIWA SUGU KAMA IFUATAVYO;

| NA | JINA LA MDAIWA | DHAMANA | AINA NA SEHEMU YA DHAMANA | DALALI | TAREHE |
|---|---|---|---|---|---|
| 1 | KAMILIUS MBAGO | NYUMBA | MKATABA WA MAUZIANO-MAJENGO MADIBIRA | HOLLNESS AND RESPISHERS | 21 – 12 - 2021 |
| 2 | VENANCE KABANGE | NYUMBA | MKATABA WA MAUZIANO- KABETE MADIBIRA | HOLLNESS AND RESPISHERS | 21 – 12 - 2021 |
| 3 | RAMADHAN DAUD | NYUMBA | MKATABA WA MAUZIANO- IKOGA MADIBIRA | HOLLNESS AND RESPISHERS | 21 – 12 - 2021 |
| 4 | NICHOLAUS KALINGA | NYUMBA | MKATABA WA MAUZIANO-NYAKADETE MADIBIRA | HOLLNESS AND RESPISHERS | 21 – 12 - 2021 |
| 5 | ALEX MPULULE | NYUMBA | MKATABA WA MAUZIANO-MAHANGO MADIBIRA | HOLLNESS AND RESPISHERS | 21 – 12 - 2021 |
| 6 | MDEGELWA PETWA | NYUMBA | MKATABA WA MAUZIANO-MAJENGO MADIBIRA | HOLLNESS AND RESPISHERS | 21 – 12 - 2021 |

Minada yote itafanyika mahali husika katika muda na siku ambayo itatangazwa kupitia katika vipeperushi na magari ya matangazo kutokana na idhini itayotoka kutoka katika ofisi za wakuu wa wilaya wanaohusika.

**MASHARTI YA MNADA;**
- Asilimia 25% ya bei iliyofikia italipwa papo hapo na asilimia 75% iliyosalia ilipwe ndani ya siku kumi na nne. (14). Kwa kushindwa kufanya hivyo itapelekea mnada kurudiwa tena na pesa zilizolipwa kutokurudishwa.
- Gharama za kumuhamisha mmiliki na kubadili umiliki ni juu ya mnunuzi.
- Dhamana itauzwa Kama ilivyo.

# Ajinyonga hadi kufa kwa kutotajwa misa ya shukrani

**Na Elizabeth John,** NJOMBE

WATU wawili wamefariki dunia katika matukio tofauti, likiwamo la mmoja kujinyonga baada ya kutotajwa kanisani kwenye misa ya shukrani na mwingine kukatwa mapanga kichwani na kufumuliwa fuvu baada ya kutoa ushahidi katika kesi ya migogoro ya ardhi.

Katika tukio la kujinyonga, Kamanda wa Polisi Mkoa wa Njombe, Hamisi Issah alisema, Ravan Lazaro (48), mkazi wa Ludewa, mtaa wa Kanisani B amejinyonga kwa waya kwa kile kinachodaiwa kutotajwa katika misa ya shukrani kanisani.

Kamanda Issah alisema mtu huyo na mkewe walikuwa na mtoto mwenye umri wa miaka 10 ambaye alivunjika mguu na baada ya kutibiwa hospitali na kupona walienda kanisani kutoa shukrani.

"Wakati wa shukrani padre wa kanisa alimtaja mama wa mtoto peke yake bila kumtaja baba hali iliyoleta sintofahamu na matokeo yake ameamua kujinyonga kwa kutumia waya," alisema.

Kamanda Issah aliwataka viongozi wa dini kuzingatia umuhimu wa familia kwa kuwa inajumuisha baba na mama, akitajwa mmoja matokeo yake inaleta hali kama hiyo.

Aidha, aliyeuawa kwa kufumuliwa fuvu ametambuliwa kuwa ni Daudi Kivavala (70), mkazi wa Kijiji cha Udonja, Wilaya Wanging'ombe, mkoani Njombe.

Kamanda Issah alisema tukio hilo lilitokea Desemba 5, mwaka huu saa 11:30 jioni.

Alisema Kivavala, alikuwa akiyafahamu maeneo mbalimbali ya kifamilia na alitakiwa kutoa ushahidi kwa Mwenyekiti wa kitongoji ili kumaliza mgogoro wa kifamilia, ambao hata hivyo, wanafamilia hao walionekana kutoridhika na ushahidi huo.

"Baada ya ushahidi huo kuna sintofahamu ya baadhi ya wanafamilia kutokuridhika...shahidi huyu ameuawa kwa kukatwa mapanga sehemu za kichwani mpaka fuvu limetoboka, jambo hili linasikitisha sana tusingependelea, tunasema kabisa migogoro mingi ambayo haina utatuzi inawezekana mashahidi wanapotea kwa njia kama hii iliyotokea," alisema Kamanda Issah.

Aliwataka wananchi kuridhika na uamuzi unaotolewa na viongozi wenye dhamana badala ya kujichukulia sheria mkononi.

"Mkiwa na maamuzi yenu tofauti ndiyo matukio haya yanaweza yakatokea, shahidi muhimu amekuja kutoa ushahidi na haki itendeke na baadaye amepoteza maisha," alisema.



# Mvua ya upepo yaua, yakosesha watu makazi

**Na Neema Hussein,**
KATAVI



MTOTO mmoja mwenye umri wa mwaka mmoja na nusu amefariki dunia na mwingine kujeruhiwa baada ya kuangukiwa na ukuta wa nyumba kutokana na mvua kubwa iliyoambatana na upepo.

Tukio hilo lilitokea Desemba 4, katika Kijiji cha Muungano na Kashelami Halmashauri ya Nsimbo, mkoani Katavi.

Akizungumza na Nipashe Kamanda wa Jeshi la Polisi mkoani Katavi, Ali Hamad alisema, kaya zaidi ya 40 zimekosa makazi na makanisa mawili kuezuliwa.

Hamad alisema mpaka sasa kamati ya ulinzi na usalama ya mkoa inakusudia kufika katika eneo la tukio na kuangalia jinsi ya kuwasaidia waathirika wa tukio hilo ambao wamehifadhiwa kwa ndugu, jamaa na marafiki.

Hata hivyo, Hamad alisema nyumba hizo hazikuwa na miundombinu imara ya kuhimili mvua na upepo na kutoa wito kwa wananchi kujitahidi kujenga nyumba imara ili kuepukana na matatizo kama hayo.

Kwa upande wake Annastazia John, shuhuda wa tukio hilo alisema ilikuwa muda wa saa 12 jioni, mama wa mtoto huyo alipomaliza kumwogesha na kumweka ndani ya nyumba yao baada ya mvua kuanza alitoka nje kufunga mlango wa chumba kingine na aliporudi ndani alikuta mtoto tayari kaangukiwa na ukuta huo.

Annastazia alisema baada ya mama mtu kuomba msaada kwa majirani walimtoa mtoto huyo na kumpeleka hospitali hadi umauti ulipomkuta.

# Serikali yagawa sukari ya magendo kwa wananchi

**Na Gideon Mwakanosya,**
SONGEA

SERIKALI imegawa kwa wananchi mifuko 550 ya sukari sawa na tani 11 iliyokamatwa na Mamlaka ya Mapato (TRA), mkoani Ruvuma mwaka jana, wilayani Mbinga.

Akigawa sukari hiyo, Mkuu wa Mkoa wa Ruvuma, Brigedia Jenerali Wirbart Ibuge, aliwataka wafanyabiashara kuwa waaminifu na kutanguliza uzalendo mbele kwa kulipa kodi zilizowekwa kwa mujibu wa sheria za nchi.

Aliwataka wananchi kwa kushirikiana na vyombo vya ulinzi na usalama kuimarisha ulinzi kwenye mipaka ya nchi ikizingatiwa kuwa Mkoa wa Ruvuma umepakana na Malawi na Msumbiji ambako bidhaa nyingi za magendo zinaingia na kusababisha ukwepaji wa kodi za serikali.

"Nachukua nafasi hii kumpongeza Meneja wa TRA na wafanyakazi wote wa Mamlaka ya Mapato Tanzania kwa kushirikiana na vyombo vya usalama kwa namna wanavyofanya kazi kwa lengo la kuhakikisha kodi inapatikana na mnalinda afya za mlaji kwa kuhakikisha chakula kinachopelekwa sokoni kisiwadhuru wenzetu," alisema Bridigadia Jenerali Ibuge.

Kwa upande wake Meneja wa TRA mkoani Ruvuma, Amina Ndumbogani, alisema kuwa mifuko 550 ilikamatwa ikiwa inaingizwa nchini kutoka nchi jirani ya Malawi kinyume cha sheria na taratibu za forodha.

Ndumbogani alisema kuwa sukari hiyo iliyokamatwa imegawiwa katika makundi maalumu kwenye wilaya zote za Mkoa wa Ruvuma ili kuyataja kuwa ni hospitali, Magereza, vituo vya watoto yatima na wenye mazingira magumu na shule zenye wanafunzi wenye mahitaji maalumu.

Alitoa wito kwa wafanyabiashara wote kuacha kufanya biashara ya kuingiza bidhaa nchini bila kufuata sheria na taratibu za forodha na ushuru wa bidhaa ya mwaka 2004 na 2010 chini ya Jumuiya ya Afrika Mashariki kwa kuwa ukiukwaji wowote ule wa sheria za ukusanyaji wa mapato ya serikali husababisha kukosesha serikali mapato ambayo yangesaidia katika kuleta maendeleo ya nchi.

Awali, Mkuu wa Wilaya ya Songea, Pololet Mgema, alisema matukio ya kukamatwa kwa bidhaa za magendo yanatokea mara kwa mara hasa Ziwa Nyasa kupitia Mbambabay ambako inadaiwa kuna njia nyingi za panya na kuhimiza kuimarisha doria kwenye maeneo hayo.

Akipokea msaada huo, Mrakibu Mwandamizi wa Jeshi la Magereza Emmanuel Ndyuka ambaye ni Mkuu wa Gereza la Kilimo la Kitai alisema msaada huo kwao umewapa faraja na kwasababu jeshi hilo limekuwa likijiendesha, bidhaa nyingi wananunua.


EAST AFRICAN CRUDE OIL PIPELINE

**OMBI LA KUONESHA NIA KWA AJILI YA UTOAJI WA HUDUMA SHUGHULI ZA MAZINGIRA KATIKA MRADI WA EACOP TANZANIA. KUMBUKUMBU:10007246**

Kampuni ya Kimataifa ya Mafuta na Gesi ya TotalEnergies East Africa Midstream B.V. inaalika taasisi zenye weledi na uzoefu kuonesha nia ya kutoa huduma ya shughuli za mazingira katika mradi wa EACOP Tanzania.

Mradi wa EACOP unahusisha ujenzi na uendeshaji wa bomba litakalofukiwa chini ya ardhi litakalovuka mipaka ya nchi mbili na litakalosafirisha mafuta kutoka eneo la Ziwa Albert nchini Uganda mpaka Pwani ya Mashariki ya Tanzania kwa ajili ya kusafirisha mafuta hayo kwenda katika masoko ya Kimataifa. Bomba hili litaanzia Kabaale katika wilaya ya Hoima nchini Uganda, mpaka Chongoleani, Mkoani Tanga nchini Tanzania. Urefu wa Bomba ni kilomita 1,443, kati ya hizo, kilomita 1,147 zitakuwa Tanzania.

Miundo mbinu itakayojengwa juu ya ardhi kwa Tanzania itahusisha vituo 4 vya pampu, vituo 2 vya kupunguzia kasi ya mtiririko wa mafuta; kituo kikuu cha kuhifadhia mafuta karibu na bahari (Marine Storage Tank) na kituo cha kupakilia mafuta (Load Out Facility); kambi 12 za wafanyakazi na kuhifadhia mabomba, barabara za kuelekea kwenye vituo na makambi; na vituo vya kuvunia mwanga wa jua (solar farms).

**MAELEZO MAFUPI KUHUSU MAWANDA YA HUDUMA:**

Mradi wa EACOP unahitaji watoa huduma wenye uzoefu na uwezo yakinifu wa kutoa huduma za shughuli za mazingira katika mawanda mbalimbali ya mradi ambayo yatahusisha:

- Tathmini ya athari za mazingira na jamiii pamoja na kuandaa taarifa za madhara hayo.
- Utafiti wa taarifa za msingi za mazingira-nchi kavu na baharini.
- Kutengeneza na kuwasilisha mpango mbadala wa bioanuai pamoja na tathmini na usimamizi wa pamoja wa huduma za mfumo wa ikolojia wa nchi kavu na baharini, ukusanyaji wa taarifa na maendeleo ya mkakati wa usimamizi.
- Kutengeneza na kutekeleza programu za kutunza na kuhifadhi mali asili za kijamii.
- Ufuatiliaji na uthibiti wa taarifa za mazingira kufuatana na sheria zilizopo.
- Kuandaa leseni na vibali vya mazingira.
- Huduma ya kuwasilisha taarifa za mazingira.
- Ukaguzi wa kuangalia utaratibu na utekelezaji wa sheria za mazingira.
- Ushauri wa jumla kuhusu mada mbalimbali za mazingira.

**VIGEZO MUHIMU:**

- Uthibitisho wa uzoefu, utendaji, na uwezo katika kutekeleza kazi za huduma za kimazingira katika mawanda ya kazi, kwa viwango vya juu nchini Tanzania, kwa kufuata viwango vya kitaifa na kimataifa (ikiwa ni pamoja na Viwango vya Shirika la Fedha la Kimataifa (IFC), na uzoefu wa angalau miaka 5 katika utendaji wa huduma kama hizo ndani ya Tanzania au Kimataifa.
- Uthibitisho wa watendakazi husika wenye vigezo na uzoefu wa hali ya juu katika kufanya tathmini ya athari za mazingira na jamiii pamoja na kuandaa taarifa za madhara hayo katika miradi ya mafuta na gesi.
- Uzoefu wa kufanya tathmini ya athari za mazingira na jamiii ambao unakidhi vigezo na mahitaji ya IFC and EP IV.
- Uwezo wa kifedha wa kutoa huduma inayotakiwa ikihusishwa na mawasilisho ya taarifa ya kifedha (financial accounts) kwa Mwaka 2020.
- Inashauriwa, muonesha nia atume maombi ya kusajiliwa na kanzi data ya EWURA (LSSP) kama mtoaji na msambazaji wa huduma ndani ya nchi wakati wa kuwasilisha ombi la kuonesha nia ya kutekeleza shughuli za progamu.
- Kuzingatia Kanuni za maudhui ya Ndani za mwaka 2017 pamoja na tafsiri ya Kampuni ya Ndani.
- Uthibitisho wa sera ya ndani ya Ubora, Afya, usalama na Mazingira, taratibu na mchakato kulingana na viwango vya ndani vya viwanda vya kazi husika.
- Uthibitisho wa usajili katika mamlaka husika ndani ya nchi kwa ajili ya utoaji wa huduma husika.
- Uthibitisho wa usajili wa Mamlaka ya Mapato Tanzania (TRA) pamoja na cheti cha uthibitisho wa kulipa kodi kwa mwaka wa fedha uliopita.

Taasisi zenye nia ya kuleta maombi na ambazo zina uwezo na rasilimali za kutekeleza shughuli au kazi zilizoorodheshwa hapo juu zinapaswa kueleza nia yao kwa lugha ya kiingereza pamoja na kuambatanisha nyaraka zilizotajwa hapo juu kupitia barua pepe kwa **eacoptz.eoi.1000001@totalenergies.com** (ukubwa wa barua pepe 20 Mb) saa au kabla ya saa **11** jioni za Afrika Mashariki (EAT) tarehe **20 Disemba 2021.** Kichwa cha barua pepe kiwe ni **10007246.**

**Muhimu:** Mradi wa EACOP utapitia na kuchambua nyaraka zilizotumwa na taasisi zitakazoonyesha nia iii kutengeneza orodha ya taasisi za awali zenye vigezo vinavyotakiwa. Taasisi zitakazokidhi vigezo iu ndiyo zitapokea na kusaini Makubaliano ya Utunzaji wa Taarifa (NDA) pamoja na mwaliko wa kuwasilisha zabuni katika kuendeleza mchakato wa zabuni.

TOLEO MAALUM

# MIAKA 60 YA UHURU WA TANGANYIKA,

### Utangulizi

Shirika la Maendeleo la Kimataifa la Japani (JICA) ni shirika ambalo linatekeleza miradi ambayo infaadhiliwa na Serikali ya Japani (ODA) ) katika nchi zaidi ya 150 zinazoendelea. Shirika hili lina ofisi katika nchi zaidi ya 100 na katika maeneo 90 duniani. JICA ni shirika kubwa zaidi linalosaidia nchi zinazoendelea duniani.

Kwa kuzingatia dira yake ya "Kuongoza ulimwengu kwa uaminifu", JICA inajikita zaidi kujengea uwezo nchi zinazoendelea ili ziweze kujitegemea na kuboresha maisha ya watu wa nchi husika.

Wakati Tanzania ikiadhimisha miaka 60 ya uhuru wa Tanganyika tarehe Desemba 9, 2021, JICA inajivunia kuwa mmoja wa wachangiaji wakubwa katika maendeleo ya nchi hii.

Shughuli za JICA nchini zinahusisha sekta nyingi ikiwa ni pamoja na kilimo, viwanda, miundombinu (uchukuzi na nishati), utawala bora, afya, maji n.k.

Zifuatazo ni baadhi ya shughuli ambazo JICA imezitekeleza nchini Tanzania tangu nchi hii ipate uhuru wake.

### 1. Mafunzo

Mahusiano kati ya JICA na Tanzania yalianza miaka 59 iliyopita, mwaka 1962, mwaka mmoja tu baada ya uhuru wa Tanganyika ambapo Mtanzania wa kwanza alipata nafasi ya mafunzo ya kiufundi nchini Japani. Tangu wakati huo ushirikiano uliendelea kukua na kupanuka kadri miaka ilivyosonga mbele na sasa sio tu ushirikiano wa kiufundi bali pia ushirikiano huo sasa unahusisha utoaji wa misaada na mikopo nafuu (grant aid and concessionary loans) ili kusaidia miradi mbalimbali ya maendeleo nchini.

Programu ya mafunzo ya muda mrefu na mfupi (KCCP) ni miongoni mwa miradi mikubwa ya JICA, ambayo hutoa nafasi sawa ya mafunzo kwa wakazi wa Japani na Tanzania. Hadi sasa, zaidi ya Watanzania 6,500 (baadhi yao ni viongozi wa ngazi za juu serikalini) wameshiriki katika programu za mafunzo ya JICA. Mafunzo hutolewa katika makundi mawili ambayo ni wakazi wa nchi tofauti katika kikundi kimoja au watu wa kutoka nchi moja. KCCP inashirikiana na Vyuo Vikuu, Makampuni na Mashirika yasiyo ya Kiserikali (NGOs).

Mwaka 2013, JICA ilianzisha programu maalum ya Shahada ya uzamili katika sekta ya elimu ya biashara kwa vijana barani Africa (Africa Business Education Initiative for Youth (ABE Initiative) ambapo jumla ya vijana 90 wa Kitanzania tayari wameweza kushiriki katika programu hii.

Mbali na programu za mafunzo, kuna vyama viwili vimeanzishwa kwa ajili ya kuwaleta pamoja wahitimu wote waliowezeshwa na JICA. Vyama hivyo ni Chama cha Watanzania waliosoma Japan (JATA) kilichoanzishwa mwaka 1984 na chama cha KAKEHASHI mwaka 2019 mahususi kwa ajili ya washiriki wa Mpango wa ABE Initiative.. Jukumu kubwa la vyama hivyo ni kuwaunganisha Watanzania na Wajapani kwa manufaa ya pande hizo mbili.

Wakati Tanzania ikiadhimisha miaka 60 ya uhuru wa Tanganyika, JICA inaahidi kuendelea kutoa ushirikiano wa kiufundi kupitia programu mbalimbali za mafunzo.

### 2. Miundombinu

JICA imekuwa ikiisaidia Tanzania kutatua changamoto za usafiri kwa zaidi ya miaka 40 sasa kupitia miradi mbalimbali. Miradi hiyo ni pamoja na ujenzi wa Daraja la Selander mwaka 1980, ukarabati wa barabara mitaa ya Kariakoo miaka ya 1990, ujenzi wa barabara ya Kawawa na Kilwa, uboreshaji wa barabara ya Ali Hassan Mwinyi, uboreshaji wa barabara ya Arusha-Namanga-Athi River, ujenzi wa barabara ya Dodoma-Babati, uboreshaji wa barabara za Bonga-Mayamaya, Dodoma-Iringa, Masasi-Mangaka, na Dodoma-Babati, upanuzi wa Barabara ya New Bagamoyo, uboreshaji wa Makutano ya Tazara (daraja la juu la Mfugale), ujenzi wa Daraja la Kimataifa la Rusumo mpakani mwa Tanzania na Rwanda na Namanga kwenye mpaka wa Tanzania na Kenya. Aidha mradi wa uboreshaji wa daraja la Gerezani unaoendelea jijini Dar es salaam.

Mbali na shughuli za ujenzi wa miundombinu, JICA pia imesaidia katika nyanja mbalimbali kama vile kujengea uwezo Watanzania juu ya teknolojia ya msingi katika kazi, mfumo wa matengenezo ya barabara za vijijini, uundaji wa Mpango Kabambe wa Usafiri Jijini Dar es Salaam, Uboreshaji wa Usafiri Dar es Salaam na utoaji wa huduma za ushauri kwa Sekretarieti ya Jumuiya ya Afrika Mashariki kuhusu miundombinu ya kikanda.

Miradi hii imepunguza muda na gharama za usafiri, kuongeza usalama, kupunguza ajali na kuchochea shughuli za kijamii na kiuchumi.



*Daraja la juu la Mfugale (TAZARA)*

JICA inajenga miundombinu bora, na miradi yake inatoa ajira kwa wazawa huku ikiimarisha ujuzi na uwezo wao wa kiteknolojia.

JICA inaahidi kuendelea kushirikiana na Tanzania katika kukuza maendeleo ya kijamii na kiuchumi kwa wananchi.

### 3. Afya na Unawaji Mikono

JICA inasaidia serikali kuboresha sekta ya afya kupitia programu mbalimbali ikiwa ni pamoja na kujenga uwezo kwa Hospitali za Rufaa za Mikoa, na unawaji wa mikono.

Kuhusu unawaji mikono, JICA imesambaza mabango zaidi ya 300 kwa shule za msingi katika wilaya tatu za Dar es Salaam (Ilala, Temeke na Kinondoni). Mabango yanaonyesha njia sahihi na umuhimu wa unawaji mikono kwa watoto wa shule. Pia imechapisha zaidi ya nakala 12,000 za mabango ya katuni ya 'manga' na kuyasambaza katika maeneo yenye miradi ya JICA na ofisi za umma kote nchini.

Aidha, JICA inashirikiana na taasisi isiyo ya kiserikali ya Kuhifadhi Mazingira Tanzania (ECCT) kuendesha mradi wa kuboresha usafi wa mazingira kwa unawaji mikono katika Wilaya ya Kisarawe.

Mradi wa unawaji mikono unalenga kuwakinga wanafunzi dhidi ya UVIKO-19 na magonjwa mengine ya kuambukiza. Zaidi ya wanafunzi 6,000 kutoka shule 12 na walimu wamefikiwa.

JICA inapenda kuwasihi wanafunzi kuzingatia kauli mbiu yetu ya "Tokomeza magonjwa kwa kunawa mikono mara kwa mara".

### Hitimisho

JICA inajali sana maendeleo ya Tanzania na watu wake, lakini pia utayari wa nchi hii na mapokezi yake katika ushirikiano unavutia.

JICA pia ina programu ya wataalam wa kujitolea, yaani, 'Japan Overseas Cooperation Volunteers (JOCV)' ambayo inalenga kutoa usaidizi wa kitaalamu katika nchi zinazoendelea. Mtaalamu wa kwanza kutoka Japani kuja Tanzania alifika mwaka 1967.

Watalaamu hao hufanya kazi na wenyeji katika sekta za kilimo, misitu, uvuvi, uhandisi wa majengo, usanifu, viwanda, ufundi stadi, afya, elimu, utalii, michezo nk.

Mpaka sasa, jumla ya wataalamu 1,700 wa kujitolea kutoka Japani wameshafanya kazi nchini huku watalaamu wa kujitolea wengine 60 walilazimika kurejea Japani mwaka jana kabla ya kumaliza muda wao wa kazi kutokana na janga la Uviko – 19.

Aidha, kwa kuwa Tanzania imebarikiwa kuwa na ardhi kubwa yenye rutuba na uoto wa asili, JICA inatoa msaada katika sekta ya kilimo na viwanda ili kukuza uchumi.

Katika kilimo, JICA imekuwa ikiwasaidia wakulima wa mpunga tangu mwaka 1974, katika mradi wa Kuendeleza Kilimo Kilimanjaro (KADP), Skimu ya Umwagiliaji ya Lower Moshi, na Kituo cha Mafunzo ya Kilimo Kilimanjaro (KATC) kwa kutoa mikopo na utaalamu kwa wakulima. Zaidi ya wakulima 15,000 wamepatiwa mafunzo na kuwezeshwa teknolojia bora za kilimo cha mpunga kupitia Mradi wa Maendeleo ya Sekta ya Mpunga (TANRICE2).

JICA pia inatekeleza Mradi wa Uwezeshaji na Ukuzaji wa Kilimo cha Mazao kwa Wakulima Wadogo (SHEP), ambao unalenga kubadilisha mawazo ya wakulima kutoka "Kuzalisha na Kutafuta soko" hadi "Kutafuta soko kabla ya kuzalisha", yaani 'Anzia Sokoni, Malizia Shambani'. Kwa kushirikiana na serikali, mpango huu umevifikia vikundi 56 vya wakulima katika Mikoa ya Arusha, Kilimanjaro, na Tanga.

JICA pia inasaidia nchi kufikia ndoto yake ya kuwa nchi ya uchumi wa viwanda ifikapo 2025 kupitia 'Mradi wa Kuimarisha Biashara za Viwanda kupitia Uzalishaji Bora na Tija (KAIZEN)' katika sekta ya viwanda. Kupitia mradi huu, uzalishaji uliimarika kwa kiasi kikubwa katika makampuni zaidi ya 100 ya Tanzania ambayo yanatumia falsafa ya "KAIZEN" huku wengine wakipunguza kiwango cha dosari viwandani kwa takriban asilimia 70.

(Angalizo: KAIZEN ni neno la Kijapani linalomaanisha "uboreshaji" na sasa linatumika duniani kote kama dhana ya uboreshaji wenye tija, kuhakikisha ubora na usalama katika mazingira ya kazi kupitia mchakato shirikishi wa utatuzi wa changamoto unaofanywa na vitengo mbalimbali kwa pamoja).

Wakati Tanzania ikijiandaa kusherehekea miaka 60 ya uhuru wa Tanganyika, JICA, kama kawaida, inaendelea kusaidia maendeleo ya nchi hii kwa njia mbalimbali kwa manufaa ya wananchi wa Tanzania na wa Japani.



*Watoto wa shule wakinawa mikono Ili kujikinga na UVIKO -19 pamoja na magonjwa mengine.*

Nipashe
MWANGA WA JAMII

# Taabu usafiri mabasi idhibitiwe mwezi huu

**KILA** Desemba tumekuwa tukishuhudia kero na taabu ya usafiri wa mabasi katika maeneo mengi hususan kutoka Dar es Salaam kwenda mikoa ya kaskazini.

Hali hii hutokana na watu wengi kwenda kusherehekea siku za mwisho wa mwaka za Krismasi na Mwaka Mpya kwenye maeneo wanayotoka, hivyo kuwapo mahitaji makubwa ya vyombo vya usafirishaji hususan mabasi.

Kutokana na hali hiyo, wenye mabasi hukiona kipindi hicho kama fursa kwao ya kutengeneza fedha nyingi na kuamua kupandisha nauli mara dufu, waliamini kuwa lazima abiria watalipa.

Kutokana na mazoea hayo, tunaona kuwa hali hiyo itajirudia kuanzia siku chache zijazo kwa kuwa zimebakia takribani wiki mbili watu wengi kuanza safari kwenda kusherehekea sikukuu hizo.

Wamiliki na wafanyakazi wa mabasi ya abiria yanayosafiri kati ya mikoa na mikoa wameshaanza kujiandaa kunufaika kwa fedha nyingi kupitia kupandisha nauli mara dufu.

Serikali katika miaka ya karibuni imekuwa ikijitahidi kuingilia kati kuhakikisha kuwa wananchi hawaumizwi na vitendo hivyo. Mojawapo ya hatua hizo ni kuruhusu magari madogo kusafirisha abiria kwa kipindi hicho.

Hata hivyo, wakati mwingine magari hayo hayatoshelezi mahitaji, hivyo wasafiri kuendelea kuteseka kwa kukwama kusafiri au kutozwa nauli ya ulanguzi.

Pamoja na kuipongeza serikali kwa kuliona tatizo hilo na kuamua kuingilia kati, lakini tunaona kwamba ipo haja ya kuchukuliwa hatua zaidi kwa lengo la kulitafutia tatizo hilo ufumbuzi wa kudumu.

Miongoni mwa hatua za kuchukua ni mamlaka husika kuhakikisha hakuna basi la abiria linalopandisha nauli kipindi chote cha sikukuu hadi Januari hivyo kuendelea kusisitiza kutumika nauli elekezi.

Pili kutoa adhabu kwa mujibu wa sheria kwa basi lolote la abiria litakalobainika kupandisha nauli kipindi hicho au kukataa kusafirisha abiria kwenda katika maeneo ambayo limesajiliwa kufanya shughuli za usafirishaji.

Pia kutoa vibali vya muda kwa wasafirishaji zaidi wenye mabasi na magari mengine yanayoweza kusafirisha abiria kwa lengo la kutosheleza mahitaji.

Tunashauri kwamba serikali iangalie uwezekano wa kuongeza safari za treni kwenye mikoa yenye mahitaji makubwa ya usafiri katika kipindi hicho hususan mikoa ya kaskazini.

Ni matarajio yetu kwamba kwa kufanya hivyo usumbufu, taabu na mateso kwa wasafiri katika kipindi hicho itabaki kuwa historia.

Tunaelewa kwamba jukumu la serikali si kuingilia soko katika mfumo wa soko huru, lakini inawajibika kufanya hivyo kwa kuingilia kwa muda mfupi pale inapoona kuna athari kwa ajili ya kuweka mambo sawa.

Kwa hiyo serikali itaonekana kwa wananchi haiwajibiki ikiwa itakaa kimya huku baadhi ya watu wakikiuka sheria kwa makusudi na kuwaimiza wananchi.

Nipashe hutolewa na kuchapishwa na:
THE GUARDIAN LIMITED
**Mhariri Mtendaji :** Beatrice Bandawe
**Meneja Usambazaji na Masoko:** Emmanuel Lyimo, 0716 500500
**Mapokezi:** 0745 700710
**Matangazo:** 0782 253676
**Baruapepe:** advertise@guardian.co.tz
**Website:** www.ippmedia.com
www.epaper.ippmedia.com




## Muungwana Lazima Nilonge



# Tanzania inavyopendeza kielimu miaka 60 Uhuru

Na Sabato Kasika

**TANGU** mwaka 1961 Tanzania ilipopata Uhuru, yapo maendeleo mengi ambayo taifa limeyafikia, katika nyanja mbalimbali kutokana na mapambano dhidi ya maadui watatu waliotangaziwa vita mara tu baada ya uhuru.

Ni ujinga, maradhi na umaskini adui waliokuwa vikwazo kwa maendeleo ya Watanzania, Rais wa kwanza Mwalimu Julius Nyerere, alianza nao kwa kuwekeza katika elimu ili kuwamaliza wengine wawili waliobakia yaani umaskini na maradhi.

Lengo la kufanya hivyo, lilikuwa ni kuachana na elimu ya kikoloni ambayo ilikuwa na ubaguzi na haikuwahakikishia Watanzania fursa za kuelimika.

Hatua ya kuwaunganisha Watanzania kuwa wamoja, ilichochangia kufanikisha harakati za kupambana na maadui kwa kumwezesha kila mmoja kwenye eneo lake kushiriki katika vita iliyokuwa inamlenga adui ujinga na sasa tunapoadhimisha miaka 60 ya uhuru, matunda yake tunayaona.

Mojawapo ya matunda hayo ni elimu, takwimu za Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Ufundi, zinaonyesha kuwa, wakati nchi inapata uhuru, ilikuwa na shule za msingi 3,270 zilizosajiliwa.

Leo taifa linapoadhimisha miaka 60 ya uhuru, kuna shule 18,546, huku 16,656 kati ya hizo zikiwa ni za serikali na 1,890 za binafsi, jambo ambalo ni la kujivunia kwa Watanzania.

Mafanikio mengine ya kujivunia katika elimu, ni uwingi wa shule za sekondari, kwa kuwa wakati nchi inapata uhuru, zilikuwapo 41 pekee huku mbili kati ya hizo zikiwa za binafsi sasa zimefikia 5,460.

Sekondari za serikali kati ya hizo ni 3,983, za binafsi zikiwa ni 1,287, na kuongezeka kwa shule hizo, kunakwenda sambamba na uandikishaji wa wanafunzi wa elimu ya sekondari kuongezeka.

Historia inaonyesha, wanafunzi wa kidato cha kwanza mwaka 1961 walikuwa ni 4,432, na kwamba mwaka huu wameandikishwa 803,085, idadi inakwenda sambamba na ongezeko la watu, lakini uelewa wa umuhimu wa elimu.

Vilevile kwa mujibu wa Waziri wa Elimu Profesa Joyce Ndalichako, vyuo vikuu vinavyopokea wanafunzi wenye mahitaji maalum vimeongezeka kutoka Chuo Kikuu kimoja cha Dar es Salaam mwaka 1961 hadi vyuo vikuu 11 mwaka 2021.

Kwa hatua ambazo nchi imefikia katika maendeleo ya elimu, ninadhani ni muhimu Watanzania kushirikiana zaidi na serikali kuondoa vikwazo vinavyokwamisha maendeleo ya elimu kwa watoto wote.

Msisitizo unaoelezwa na serikali katika kuimarisha elimu, ni zaidi katika masuala ya Teknolojia ya Habari na Mawasiliano (TEHAMA), Sayansi, Ujasiriamali na stadi za kazi mtambuka, huku kukiwa na fani za kimkakati.

Fani hizo za kimkakati miongoni mwake ni uhandisi, kilimo, udaktari, kwamba zinapewa kipaumbele, huku serikali itaendelea kuboresha miundombinu ya shule, ili kutoa fursa zaidi kwa watoto wa kike na wa kiume.

Hivyo, ni vyema wazazi na walezi nao wakahakikisha watoto wao wanapata elimu bila ubaguzi au upendeleo ili hatimaye kila mmoja wao awe na mchango kwa maendeleo yake na ya taifa kwa kutumia elimu aliyopata.

Miaka 60 elimu imetoka kule sasa ipo hapa, kilichobaki ni kuendelea kuboresha zaidi mazingira ya shule ili yawe rafiki hata kwa watoto wa kike ambao wamekuwa wakikumbana na matatizo mengi.

Katika juhudi za kutatua changamoto za watoto wa kike, serikali imeshaanza kujenga shule 274 za kutwa, huku 10 zikiwa ni za wasichana.

Hivi karibuni imetoa Shilingi bilioni 1.4 kwa ajili ya kufanikisha kazi hiyo na kukamilisha kazi hiyo.

# TRA yatoa elimu ya mlipakodi Zanzibar mlango kwa mlango

**Na Mwandishi Wetu**

MAMLAKA ya Mapato Tanzania (TRA) kwa kushirikiana na Bodi ya Mapato Zanzibar (ZRB), wameanza kampeni ya elimu kwa mlipakodi mlango kwa mlango Zanzibar kisiwani Unguja.

Kampeni hiyo inatarajiwa kufanyika kwa siku tano kuanzia Desemba 4 hadi Desemba mwaka huu.

Kampeni inalenga kutoa elimu kwa walipakodi ili kuwajengea uelewa wa kutosha juu ya masuala mbalimbali yanayohusu kodi, kusikiliza maoni yao kwa ajili ya kuboresha huduma za kikodi, kuwakumbusha kulipa kodi stahiki na kwa wakati kusikiliza kero na vikwazo walivyonavyo na kuvitafutia ufumbuzi.

Kampeni hiyo ilifunguliwa rasmi Desemba 4, mwaka huu na Naibu Kamishna wa TRA Zanzibar, Juma Bakari Hassan, ambapo katika ufunguzi huo aligusia masuala mbalimbali ikiwamo kutatua vikwazo kwa wafanyabiashara waliotembelewa na kupata taarifa sahihi kwa ajili ya kusajiliwa kwa wale ambao hawajasajiliwa.

Vilevile, aliwahimiza maofisa wa TRA kutumia lugha nzuri na kuwaelimisha walipakodi kwa ufasaha juu ya wajibu na haki zao, kuzingatia weledi na uwajibikaji na uadilifu.

Pia aliwashukuru viongozi wa ngazi mbalimbali wa Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar kwa ushirikiano waliotoa katika maandalizi na utekelezaji wa kampeni hiyo ya elimu ya kodi mlango kwa mlango.

TRA imeendesha kampeni hiyo katika mikoa karibu yote ya Tanzania Bara, ikibainisha kuwa imekuwa na mafanikio makubwa katika kuimarisha biashara na makusanyo ya mapato.




Naibu Waziri wa Fedha na Mipango, Mhandisi Hamad Yussuf Masauni, akionyesha kitabu alichokizindua wakati wa hafla ya uzinduzi wa Tamasha la Kitakwimu (Data Tamasha 2021) kuhusu matumizi ya takwimu kwenye uchumi wa kidijitali lililofanyika jijini Dar es Salaam. **PICHA: JOSEPHINE MAJURA**

# PPRA yatakiwa kurahisisha utoaji wa huduma

**Na Idda Mushi,** MOROGORO

MAMLAKA ya Udhibiti wa Ununuzi wa Umma (PPRA) imetakiwa kushirikiana na taasisi nyingine za serikali ikiwamo Wizara ya Fedha na Mamlaka ya Serikali Mtandao (EGA) kuunda mfumo binafsi unaojitegemea ili kurahisisha utoaji wa huduma na kupunguza gharama za uendeshaji.

Katibu Mkuu Ofisi ya Rais Utumishi, Dk. Laurean Ndumbaro, alisema hayo alipokutana Morogoro na watumishi wa mamlaka hiyo.

Alisema kwa kuwa na mfumo wake unaojitegemea badala ya kutegemea mifumo ya nje, itarahisisha kuuboresha kulingana na mahitaji yaliyopo na kupunguza gharama za uendeshaji.

"Wakati wote Rais Samia Suluhu Hassan amekuwa akisisitiza mamlaka na taasisi mbalimbali kuwa na mifumo yake ya msingi yenyewe, na mifumo mingine midogo midogo hata ikiwa ya kutoka nje ya nchi sio mbaya, lakini mifumo mikuu ya msingi iwe ni ya mamlaka au taasisi husika," alisisitiza.

Akawahimiza watumishi hao wa PPRA na wengine wa umma, kutambua dhamana waliyoaminiwa na kupewa kwa kutekeleza majukumu yao kwa weledi na ufanisi mkubwa, alishauri uboreshwaji wa kanuni zake ili kuangalia suala la mishahara, posho na maslahi ya wafanyakazi.

Ofisa Mtendaji Mkuu wa PPRA, Dk. Irene Isaka, alisema katika mwaka wa fedha uliomalizika, wamepitia ununuzi wa umma wa thamani ya Sh. trilioni 9.2, huku asilimia 90 ikiwa ni kutoka kwa wanunuzi wakubwa.

Aidha, alisema katika kipindi hicho walifanya kaguzi za ununuzi wa thamani ya Sh. trilioni 5.7, kukagua mikataba 282 na ununuzi kwa njia ya kimtandao ukiongezeka kufikia taasisi 718 mwaka uliopita wa fedha tofauti na taasisi 509 zilizokuwapo awali na kushauri kwa utaalamu na kisheria wanunuzi 471.

"Katika kipindi hicho tuliweza kupata matumizi ya taarifa 31,423 zilizochakatwa kutoka kwenye mfumo wa ununuzi wa umma kwa njia ya mtandao, TANePS, ikilinganishwa na taarifa 17,200 za kipindi kilichopita," alisema ofisa mtendaji mkuu huyo wa PPRA.

Dk. Isihaka alisema licha ya mamlaka hiyo kupata hati safi katika mwaka uliopita wa fedha, bado wamekusudia kufanya upekuzi kwa wafanyakazi wake ili kuongeza na kuboresha uwazi na uwajibikaji wa utendaji kazi wa mamlaka hiyo na Desemba 14 watakutana na watumishi wote wa mamlaka hiyo.


## Viwango Vipya vya Kuzuru (Roaming) na Vodacom kwa Uingereza

**A. Lipa kadiri utumiavyo: viwango vya sasa vya kupokea simu**

| | Viwango vya sasa (Pamoja na kodi) | |
|---|---|---|
| Mtandao | Nchi | Kupokea Simu (Dk) |
| Vodafone | UK | Tsh. 500 |

**B. Lipa kadiri utumiavyo: Mabadiliko ya viwango vya kupokea simu**

| | Viwango vipya (Pamoja na kodi) | |
|---|---|---|
| Mtandao | Nchi | Kupokea Simu (Dk) |
| Vodafone | UK | Tsh. 1,100 |

Viwango hivi vitatumika kwa watumiaji wa malipo ya baadae, watumiaji mseto na watumiaje wa malipo ya awali kodi zote zikijumuishwa.
Kwa maelezo zaidi tembelea: https://vodacom.co.tz/international-roaming

Pamoja tunaweza


# Waziri akipa changamoto Chuo cha Ardhi Tabora

**Na Munir Shemweta,** TABORA

Naibu Waziri wa Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi, Dk. Angeline Mabula, amekitaka Chuo cha Ardhi Tabora (ARITA) kuitangaza idara yake ya uchapishaji ili kufahamika na kutumika kwa shughuli za uchapishaji yakiwamo machapisho ya serikali.

Dkt Mabula alisema hayo Jumapili alipofanya ziara ARITA kukagua utendaji kazi akiwa kwenye ziara ya kikazi mkoani Tabora.

Kwa mujibu wa Mabula, Chuo cha Ardhi Tabora kinatakiwa kijitangaza hasa idara yake ya uchapishaji kwa kuwa kazi za idara hiyo zinaweza kukiingizia mapato chuo itakayoweza kutumika katika shughuli mbalimbali za maendeleo ya chuo.

"Tungetumia sehemu ya printing ya chuo hiki tungweza kupata fedha nyingi, hivyo tunatakiwa tuitangaze idara hii ya uchapishaji kwa kuwa Ofisi ya Mpiga Chapa Mkuu wa Serikali haiwezi kufanya kazi zote na pale ofisi hiyo itakapozidiwa basi chuo hicho kifanye kazi hiyo,". alisema.

Mkuu wa idara ya Sanaa, Ubunifu na Uchapishaji wa Chuo cha Ardhi Tabora, Praygod Lema, alimueleza Naibu Waziri kuwa, idara hiyo pamoja na kufanya kazi kubwa ya uchapishaji baadhi ya nyaraka za Wizara ya Ardhi na za halmadhauri ya jiji la Dodoma bado ina changamoto ya mashine ya uchapishaji kutokana na zilizopo sasa kutoendana na kasi ya mahitaji ambapo aliomba idara hiyo kupatiwa mashine nyingine ya kisasa.

"Pamoja na changamoto mlizokuwa nazo kuna haja ya kufanya matangazo na mnaweza kutumia hata vyombo vya habari ili muweze kupata kazi na kuingiza fedha maana bila ya hivyo mtaendelea kuwa na changamoto za kifedha, " alisema Dk. Mabula.

Hata hivyo, alikipongeza Chuo kwa kazi nzuri pamoja na changamoto inazozikabili katika utendaji kazi wake na kuutaka uongozi wa chuo kufuatilia maombi mbalimbali inayoyapeleka Wizarani kwa ajili ya kusaidiwa.

Mkuu wa Chuo cha Ardhi Morogoro, Donald Rweramila, alisema, pamoja na ARITA kufanya kazi ya uchapishaji lakini hakina maabara ya fani ya Sanaa, Ubunifu na Uchapishaji kwa ajili ya mafunzo ya vitendo, jambo alilolieleza kuwa linawafanya wanafunzi kutumika zaidi uandani.

HABARI KITAIFA

## PSSSF yatwaa tuzo ya umahiri

**Na Mwandishi Wetu**

MFUKO wa Hifadhi ya Jamii kwa Watumishi wa Umma (PSSSF) umetwaa Tuzo ya Umahiri katika Uwasilishaji wa Taarifa za Mahesabu kwa mwaka 2020.

Akizungumza baada ya kupokea tuzo hiyo katika hafla ya kufunga mafunzo pamoja na utoaji wa tuzo za umahiri katika uandaaji wa Taarifa za Fedha ya Mwaka 2020 (Best Presented Financial Statements for the Year 2020 Awards) kwa Taasisi, kampuni pamoja na mashirika zinazotolewa na Bodi ya Taifa ya Wahasibu na Wakaguzi wa Hesabu Tanzania (NBAA) zilizofanyika katika hoteli ya APC Bunju jijini Dar es Salaam juzi, Mkurugenzi wa Fedha, PSSSF, Beatrice Musa Lupi, alisema ushindi huo ni ishara ya kwamba PSSSF inaandaa mahesabu kwa kuzingatia vigezo vilivyowekwa kimataifa na inaashiria uwepo wa weledi wa tasnia husika kwa upande wa watumishi.

"Sambamba na hayo niliyoyasema, pia inaashiria uwapo wa usimamizi makini wa fedha za wanachama na hii inatupatia heshima kama taasisi," alisema.

Aliwahakikishia wanachama dhamira ya PSSSF kuhakikisha usalama wa michango yao unazingatiwa kwa kiwango cha juu wakati wote, ikiwamo uwazi kwenye usimamizi na utunzaji wa rasilimali za mfuko.

"Ushindi huu pia unaashiria uwapo wa kesho ya wanachama wetu kama kaulimbiu yetu inavyosema Leo, Kesho, Pamoja," alihitimisha Beatrice.

## OSHA yawanoa wakaguzi wake

**Na Frank Monyo**

WAKALA wa Usalama na Afya Mahali Pa Kazi (OSHA) umewapa mafunzo wakaguzi wa kada mbalimbali wanaofanya kazi chini ya taasisi hiyo.

Lengo la mafunzo hayo ni kuwaongezea weledi katika shughuli zao za ukaguzi ili kuleta tija kwa taifa kwa kuhakikisha maeneo yote ya kazi yanakaguliwa ipasavyo na yanazingatia sheria Na.5 ya mwaka 2003 ya usalama na afya na kanuni zake.

Akifunga mafunzo hayo ya siku tano mwishoni mwa wiki, mkoani Morogoro, Mtendaji Mkuu wa OSHA, Khadija Mwenda, aliwataka wakaguzi kutoka OSHA kuzingatia uadilifu, tunu za taasisi na miiko ya utumishi wa umma wakati wote wanapotekeleza majukumu yao.

"Dira yetu inataka maeneo yote ya kazi yawe salama na yenye afya, hivyo tutahakikisha tunawakagua na kuwashauri wadau wetu waweze kukidhi matakwa ya sheria ya usalama na afya mahali pa kazi.

"Kupitia mafunzo haya tume kumbushana namna ambavyo serikali yetu iko makini kuhakikisha vitendo vya rushwa vinazuiwa kwa sababu rushwa inauza haki hivyo basi unapopokea rushwa katika eneo la kazi unauza utu na usalama wa wafanyakazi."

Alisema pia wamewafundisha weledi wa kutambua vihatarishi vya ajali katika maeneo ya kazi na jinsi gani waweze kutoa ushauri juu ya namna ya kuviondoa vihatarishi hivyo.

# Sababu baadhi maeneo Tanzania kutoingia kwenye urithi wa dunia

**Na Beatrice Shayo**

SERIKALI imesema baadhi ya maeneo ikiwamo ya kihistoria, utamaduni na mambo ya kale ya Tanzania yanashindwa kuingia kwenye urithi wa dunia kutokana na kukosekana kwa ujuzi wa kutetea vigezo vinavyohitajika na Shirika la Umoja wa Mataifa la Elimu, Sayansi na Utamaduni (UNESCO).

Hayo yalisemwa jijini Dar es Salaam na Naibu Waziri wa Maliasili na Utalii, Mary Masanja wakati akifungua mkutano wa wiki mbili uliyowakutanisha wataalamu kutoka barani Afrika wanaohusika na masuala hayo ya historia, utamaduni na mambo ya kale ili kujengewa uwezo wa kutetea maeneo yao ya kale yaweze kuingizwa kwenye urithi wa dunia.

Masanja alisema yapo maeneo ya kihistoria Tanzani kama watumwa walipopita na kuacha nyayo zao wanapaswa kuingizwa kwenye urithi wa dunia, hivyo mafunzo hayo yakifanyika vizuri na wataalamu wakapata ujuzi wa kutosha wataweza kutetea maeneo hayo kisha kutambulika kidunia na kuvutia watalii wengi zaidi.

Alisema mpaka sasa Tanzania ina maeneo saba yaliyoingia kwenye urithi wa dunia ambayo ni Hifadhi ya Taifa ya Serengeti, Ngorongoro, Selous, Kilwa Kisiwani na Songomnala, Mlima Kilimanjaro, Michoro ya Miamba Kondoa na Mji Mkongwe Zanzibar.

"Tanzania ina maeneo mengi ambayo hajaingia kwenye urithi wa dunia, tunamatumaini kuwa kupitia mafunzo haya wataalamu wetu wataelimika na kupata ujuzi wa kutosha kuhakikisha tunayaingiza maeneo yetu ili kuvutia watalii wengi zaidi kuja nchini," alisema.

Aidha, Masanja amewataka Watanzania kuendelea kuizungumzia Tanzania kwa mambo mazuri ili kuvutia watalii kuja nchini na sekta ya utalii iweze kuwa namba moja katika kuchangia pato la Taifa.

Mratibu wa mafunzo hayo, James Mwakipala, alisema nchi inapofanikiwa kuingia maeneo yake katika urithi wa dunia inasaidia kufahamika kidunia na kuirahisishia nchi kupata watalii wengi.



Meneja wa Fedha wa Kampuni ya TBL, Fredy Kayanda, akipokea tuzo ya mshindi wa kwanza wa umahiri katika kuwasilisha taarifa za mahesabu kwa mwaka 2020 kutoka kwa Mhasibu Mkuu wa Serikali, Leonard Mkude (kushoto), zilizotolewa na Bodi ya Taifa ya Uhasibu na Ukaguzi wa Hesabu (NBAA) katika hafla iliyofanyika jijini Dar es Salaam mwishoni mwa wiki. TBL imeibuka mshindi wa kwanza katika sekta ya viwanda. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# 'Wakusanya kodi tegemeo kupaa mapato ya ndani'

**Na Christina Mwakangale**

SERIKALI imesema ongezeko la mapato ya ndani linawategemea wataalamu wa ukusanyaji kodi na ushuru wa forodha pamoja na ushirikiano kutoka kwa walipakodi.

Naibu Katibu Mkuu Wizara ya Fedha na Mipango, Adolf Ndunguru, aliyasema hayo mwishoni mwa wiki kwenye mahafali ya 14 ya Chuo cha Kodi (ITA), mkoani Dar es Salaam na kutunuku vyeti vya ngazi na fani tofauti kwa wahitimu 387 katika mwaka wa masomo 2020/21.

Alisema ili kutatua vikwazo vilivyopo katika ukusanyaji kodi na kuondokana na utegemezi wa fedha za wahisani, wahitimu hao wayatumie mafunzo waliyoyapata kwa kuwa wabunifu, kutoa elimu na kujenga mahusiano mazuri kwa walipakodi.

"Tunawategemea wahitimu kwenye taaluma ya forodha na kodi ili kutatua changamoto za ukusanyaji kodi, pia serikali inaandaa fursa ili mpate shughuli za kufanya. Mafunzo ya forodha, kodi yamekuza mapato ya ndani na kupunguza utegemezi kutoka kwa wahisani katika kugharamia huduma," alisema Ndunguru.

Kuhusu ongezeko la mapato nchini, Ndunguru alisema chuo hicho kimesaidia kutoa wahitimu ambao wanatumika kutoa elimu ya kodi, ili kukuza uchumi na kupata maendeleo ya watu kupitia upatikanaji wa huduma za kijamii.

"Kutoza kodi na kukusanya mapato ni suala linalohusisha wadau wengi, hivyo iwepo elimu ya kutosha. Serikali inapoteza mapato kutokana na wataalamu wachache nchini serikalini na kwenye sekta zingine," alisema Ndunguru.

Kadhalika, alitoa wito kwa wahitimu kutumika ipasavyo ili kutoa elimu kwa walipakodi na kupunguza malalamiko kutoka kwa wafanyabiashara, pia chuo kijiimarishe katika kufanya utafiti hususani kuhusu kukusanya kodi kwenye taasisi zinazochipukia hasa uchimbaji madini kwa kuwapo mfumo bora wa ukusanyaji mapato. Mkuu wa Baraza la chuo hicho, Dk. Samwel Werema, alisema kinaiomba serikali kutenga bajeti kwa ajili ya ukarabati na ujenzi wa majengo mapya ili kukidhi mahitaji ya ukanda wa Afrika Mashariki na zingine barani Afrika.

"Jitihada za chuo ni kuongeza utaalamu wa wataalamu wa kodi, ushauri wa forodha. Wahitimu mkafuate maadili, mkawajibike na mtimize majukumu yenu kwa tija ya taifa," alisema Dk. Werema.

Kamishna Mkuu wa Mamlaka ya Mapato Tanzania (TRA), Alphayo Kidata, alisema mamlaka hiyo itaendelea kukijengea uwezo chuo hicho, ili kukifanya kituo cha umahiri na ubora kwa ukanda huo, huku akisema wanafunzi 27 waliofanya vizuri wapate fursa na kutumika na mamlaka kwa manufaa ya taifa.

# Barrick yawezesha mradi chanjo ya corona Tarime

**Na Mwandishi Wetu**

KAMPUNI ya Madini Barrick, kupitia mgodi wake wa North Mara, mkoani Mara, imefadhili mradi wa kuelimisha wananchi masuala ya afya na kupima magonjwa mbalimbali, kupata chanjo dhidi ya UVIKO-19.

Mradhi huo pia unahusu kujitolea kutoa damu, katika vijiji 11 vinavyozunguka mgodi huo uliopo wilayani Tarime mkoani Mara.

Mradi huo wa wiki 2 ulioanza Septemba 11 na kuhitimishwa Desemba 1, umetekelezwa kupitia Wizara ya Afya kupitia Mganga Mkuu wa Wilaya ya Tarime, umewafikia wananchi zaidi ya 3,000 ambao wamejitokeza kupima magonjwa ya UKIMWI, kifua kikuu, kupata chanjo ya UVIKO-19, na baadhi yao kujitolea kutoa damu kwa ajili ya Benki ya Damu, ambapo lita 159 zilipatikana, pia wananchi walipata ushauri wa kiafya kuhusiana na magonjwa mbalimbali kutoka kwa madaktari waliokuwa wanatekeleza mradi.

Akizungumza kwa niaba ya wanakijiji wenzake kuhusiana na mradi huu, Nyamwiga Warioba, mkazi wa kijiji cha Nyamongo, alisema kupitia mradi huu wananchi wengi wamepata fursa ya kupima afya zao na kupata elimu ya afya kuhusiana na maradhi mbalimbali, ameishukuru Barrick North Mara kwa kufanya uwezeshaji unaolenga kuboresha afya za wananchi sambamba na kudhamini maadhimisho ya Siku ya Ukimwi Duniani.

Mkazi wa Kijiji cha Matongo, Maria Samweli, alisema yeye pamoja na wanawake wenzake wamepata fursa ya kupima magonjwa mbalimbali na kupata ushauri kuhusiana na jinsi ya kukabiliana na magonjwa sugu yanayowasumbua wanawake wengi na watoto ambapo pia baadhi yao wamepatiwa chanjo ya UVIKO- 19.

Julius Sospeter, mkazi wa kijiji cha Nyangoto, alisema yeye na wanakijiji wenzake wamehamasika kujitolea kutoa damu kutokana na kupata taarifa kuwa wapo wagonjwa wanaohitaji kuongezewa damu. Aliomba wadau waliofanikisha zoezi hili kuhakikisha linakuwa endelevu na kufanyika mara kwa mara.

Mganga Mkuu wa Barrick North Mara, Dk. Nicholas Mboya, aliwashukuru wananchi kwa kuwa na mwamko mkubwa kushiriki zoezi hili la kupimwa afya zao na kupata ushauri wa afya kutoka kwa wataalamu ambalo limepata mafanikio makubwa. Aliishukuru serikali na taasisi mbalimbali walizoshirikiana nazo kufanikisha mradi huu ambao umewanufaisha wananchi wengi.



Mkuu wa Wilaya ya Kinondoni, Godwin Gondwe (katikati), akisikiliza maelezo kutoka kwa mzalishaji wa manukato ya nyumbani wa Taasisi ya Yorlanda Interior Designer, Yorlanda Innocent (kushoto), katika hafla ya wanawake wajasiriamali wa wilaya hiyo, ijulikanayo 'AMKA TWENDE', iliyoandaliwa na Taasisi ya Open Kitchen inayowaunganisha wanawake wajasiriamali jijini Dar es Salaam juzi. Kulia ni Mkurugenzi wa Open Kitchen, Upendo Mwalongo. **PICHA: JUMANNE JUMA**

# Makandarasi waaswa miradi ya kuwatesa

**Na Joseph Mwendapole**

BODI ya Usajili wa Makandarasi (CRB), imewataka makandarasi kuchukua miradi ya ujenzi ambayo wanaweza kuitekeleza na kuikamilisha kwa ufanisi na kwa wakati badala ya kuchukua kazi zitakazowapa mateso na kushindwa kuzitekeleza.

Hayo yalisemwa mwishoni mwa wiki na Msajili wa Bodi hiyo, Mhandisi Rhoben Nkori wakati akizungumza kwenye mafunzo ya siku tatu kuhusu usimamizi wa mikataba kwa makandarasi wazalendo.

Alisema baadhi ya makandarasi wamekuwa wakiingia kichwa kichwa kwenye mikataba ya ujenzi wanapotajiwa kiasi cha fedha bila kufanya tathmini ya kutosha na kuangalia kama mikataba wanayoingia inatekelezeka.

"Unachukua mkataba ambao unakutesa mpaka unakimbia watu, unakutana na mtu mjini akikuita jina unaogopa unajua sijui huyu atakuwa polisi maana unakuwa unaishi kwa wasiwasi kwasababu umekimbia mradi wa watu sasa kwanini ufike kote huko," alisema Nkori.

Aliwataka waliohudhuria mafunzo hayo kuelimisha na wenzao ambao hawajapata mafunzo hayo ili kwenye utekelezaji wa miradi ya ujenzi wasije kufanya makosa ambayo athari zake zitawakuta hata wale waliopata mafunzo hayo.

"Kuhusu mikataba kama alivyosema mkufunzi ukisimamia vizuri mkataba unajua haki zako na mipaka yako wajibu wako na wajibu wa aliyekupa kazi. Mwingine akiona tu fedha za mradi anauliza sehemu ya kusaini kabla hata hajasoma mkataba unasemaje, lakini baadaye anaanza kulalamika kwamba malipo yanachelewa."

"Tusome mikataba ukiona kipengele fulani hakijakaa sawa na hukieleweki mtafute mwanasheria au mhandisi au mkadiriaji majenzi akusaidie na baada ya hapo fanya mazungumzo kwamba huu mkataba hauko sawa na mimi kwa mawazo yangu ni bora ukae bila kazi kuliko kufanya kazi ambayo itakutesa sana na kusababisha uishi maisha ya kujificha ficha," alisema Mhandisi Nkori.

Naye Msajili Msaidizi wa Bodi hiyo, David Jere, alisema mafunzo hayo yamehudhuriwa na makandarasi 126 wa madaraja mbalimbali kutoka mikoa 13 ya Dar es Salaam, Morogoro, Mbeya, Mwanza, Njombe na Ruvuma. Alisema wengine walitoka mikoa ya Tabora, Arusha, Kagera, Iringa, Lindi, Shinyanga na Tanga na kwamba mafunzo ya contract management yalihusu kunoa ujuzi wa makandarasi katika usimamizi wa mikataba hasa maeneo ya vitu muhimu katika ujenzi.

Mhandisi Jere alisema makandarasi wamefundishwa kujua haki na wajibu wa kila upande kwenye mkataba, nyaraka za mkataba, hatua katika usimamizi wa mikataba, utatuzi wa migogoro na madai katika mikataba.

Alisema makandarasi pia wameelimishwa kuhusu mfumo wa manunuzi kwa njia ya kielektroniki yaani e-procurement system (TANePS), ambao ndio unatumika kwa sasa serikalini kwa zabuni zote.

Mkandarasi wa umeme wa majumbani na viwandani, Yahaya Kika aliyehudhuria mafunzo hayo alipongeza mafunzo hayo akisema kuwa yanawasaidia makandarasi kwenye maeneo mengi.

Alisema hata mfumo wa kujaza zabuni kielektroniki TANePS umekuwa ukiwasumbua makandarasi wengi hivyo mafunzo wanayopewa na CRB yamekuwa msaada mkubwa kwa makandarasi.

## Wakwama kwenda shule kisa umbali

**Na Julieth Mkireri,** KIBAHA

WANAFUNZI 50 wa Kata ya Boko Mnemela katika Wilaya ya Kibaha wameshindwa kuanza masomo ya sekondari kutokana na kushindwa kutembea umbali wa kilomita tisa.

Hayo yamebainishwa na Mratibu wa Elimu wa Kata hiyo, Haiba Sanze, alipokuwa akitoa taarifa katika harambee ya kuchangia ujenzi wa Shule ya Sekondari katika Kata ya Boko Mnemela iliyoandaliwa na Mbunge na Mbunge wa Kibaha Vijijini, Michael Mwakamo.

Alisema idadi hiyo ni kwa miaka mitatu mfululizo ambapo pia mbali ya wanafunzi hao kushindwa kuanza kidato cha kwanza, wapo zaidi ya 20 wameshindwa kuendelea na masomo kutokana na kikwazo hicho cha umbali na wazazi kushindwa kumudu kuwalipia nauli ya bodaboda kila siku.

Kutokana na hali hiyo Mbunge Mwakamo amefanya harambee kuchangia tofali na mifuko ya saruji kwa ajili ya ujenzi wa shule ya sekondari kunusuru wanafunzi wanaokosa elimu ya sekondari.

## Mbunge aishauri BoT mfumo wa biashara

**Na Thobias Mwanakatwe**

MBUNGE wa Momba mkoani Songwe, Condester Sichalwe, ameishauri Benki Kuu ya Tanzania (BoT) kuangalia njia bora na itakayofaa kuingia katika mfumo wa biashara ya 'Block chain technology' itakayo saidia kuongeza pato la taifa na kwa mtu mmoja mmoja.

Alisema hayo juzi katika mkutano mkuu wa 21 wa BoT, ambao hujumuisha wadau mbalimbali na wakuu wote wa taasisi za kifedha hapa nchini.

Alisema mfumo wa kibiashara wa Block chain technology, ni njia ya kiteknolojia ambayo taifa likiamua kuwekeza, kuna uwezekano mkubwa wa kukuza uchumi wake.


"Kwa niaba ya Watanzania wenzangu, nataka kujua ni kwanini BoT mnasuasua kuingia kwenye mfumo huu wa biashara, maana tumeshuhudia baadhi ya nchi kama vile Nigeria wamepiga hatua kubwa kupitia Block Chain Technology, lakini nashangaa nchi yetu haifanyi hivyo na inapoteza fedha nyingi sana kwa kutofanya biashara hii," alisema Sichalwe.

Gavana wa BoT, Profesa Florens Luoga, akijibia hoja hiyo, amemshukuru Sichalwe kwa maono hayo na kueleza kuwa tayari BoT kwa kushirikiana na taasisi zingine za kifedha wanautambua mfumo wa kibiashara na sasa kinachofanyika ni kutaka kuanza rasmi kuitambulisha kwa wananchi.

"Sisi kama Benki Kuu mfumo huu tunaufahamu vizuri sana na tunachokifanya hivi sasa ni kutafuta njia bora ya kuanza rasmi kufanya biashara hii," alisema Prof. Luoga.

Nipashe
# TESA
Jumanne Desemba 7, 2021
TEKNOLOJIA • ELIMU • SAYANSI

Ukurasa 13



Ukurasa 14

MSOMI: TUONGEZE NYUKLIA KWENYE KAPU LA NISHATI



RUKSA KUREJEA SHULENI KUTAOKOA MAISHA MABINTI, 'VICHANGA'


ELIMU

NA PETER ORWA

## MIAKA 60 YA UHURU

# Ijue safari ya elimu nchini toka 'Enzi za Mwalimu' hadi iliko leo

- Uandikishaji shule kipimo 'shika sikio'
- UPE na walimu mahiri elimu darasa 7
- Bure ngazi zote na bajeti 'imeshiba'



Waliokuwa wanafunzi wa Shule ya Sekondari Iyunga mjini Mbeya kati ya mwaka 1966 hadi 1969, katika picha ya pamoja zama zao. **PICHA: MTANDAO**

UNAPOTAMKA elimu, inaonekana moja kwa moja kuwapo zawadi ya kisekta kwa miaka 60 ya Uhuru.

Mwasisi wa Taifa na kiongozi mkuu wa nchi, Mwalimu Julius Nyerere, kama ilivyo taaluma yake ya msingi, miongoni mwa uzito muda wote ni kwenye sekta ya elimu.

Daima katika zama za uongozi wake na hata awamu tano zilizomrithi jukumu, sekta elimu haijawahi kukaa kando. Ni Jumapili tu iliyopita Rais Samia Suluhu Hasasan aligawa maarifa nini kifanyike katika elimu ndani ya halmashauri nchini.

Elimu ni taaluma inayobeba mustakabali kichwani kwa mtu; uelewa, maarifa pamoja na ujuzi ambao ni mtaji mkuu kwa binadamu.

Baada ya uhuru wa nchi Desemba 9, mwaka 1961, hatua ya awali kabisa kulikuwapo na tabasamu la wananchi kushangilia ikiendana na Mpango wa Maendeleo ya Tanganyika wa mpito wakati huo uliogota 1964 kulitangazwa 'elimu kwa wote' kutoka mfumo wa kitabaka.

Ni uamuzi uliotamatisha 'umimi' katika elimu kitaifa uliokuwa katika mgawanyiko, Wazungu wanapata fursa zaidi hadi elimu ya juu, kisha jamii ya waasia na kufuatiwa na wenyeji asilia mwisho.

Kuna hatua kihistoria zinajulikana sana, shule zote za kitabaka zikawa za umma pasipo vikwazo. Watawala wa zamani Uingereza walitoa fursa za masomo ya juu kuanzia mwaka 1960.

Chuo Kikuu cha Dar es Salaam (UDSM) kilikuwa tawi la Chuo Kikuu cha Afrika Mashariki iliyoundwa na Makerere (Uganda) na Nairobi (Kenya), vilinufaika na ulezi wa Chuo Kikuu cha London Uingereza.

Kila nchi ilikuwa na eneo mahsusi kitaaluma la kuendesha na katika fani zisizokuwapo katika nchi husika, wanafunzi walipelekwa jirani kusoma huko kulingana na idadi ya nafasi iliyopewa.

Mwaka 1963 nchini kuliundwa Taasisi ya Elimu Tanzania (TET), yenye jukumu kuu la kutafsiri sera ya elimu, kuweka mitaala na programu za vifaa vya kujifunzia, lengo ni kutoa elimu bora kwa ngazi ya awali, msingi, sekondari na vyuo vya ualimu.

Kisheria, TET ilipewa hadhi ya kitengo ndani ya Chuo Kikuu Kishiriki cha Dar es Salaam, chenye jukumu kuu la kuratibu kazi ya utoaji wa mafunzo ya ualimu katika chuo hicho na kusaidia Wizara ya Elimu kuboresha ufundishaji na kujifunza shuleni na kwenye vyuo vya ualimu.

Hapo pia, hapawezi kuachwa kutajwa Chuo cha Ualimu Chang'ombe, Dar es Saalam, ambayo ni zao la mchango wa marafiki wa uhuru nchi katika siku za kwanza. Hivi sasa ni sehemu ya Chuo Kikuu cha Dar es Salaam - DUCE.

**MAGEUZI YA 1964**

Hata hivyo, baada ya 1964, mwaka uliobeba historia ndefu ikiwamo nchi kuingia mfumo hodhi wa kisasa, Mpango wa Kwanza wa Maendeleo wa Miaka Mitano ulianzia; 1964 -1969, sehemu ya maudhui yake yanagusa mtazamo maalum wa kueneza kwa kina elimu ya msingi kila mahali, kwa ngazi ya kila kijiji na kitongoji ambayo mpango huo ulilenga.

Ni mazingira yaliyoendana kitaifa kuwapo lengo kubwa la wataalamu wa elimu kuanzia ngazi ya utumishi wa umma, wenye elimu ya msingi, na kufuta kundi kubwa la wasiojua kusoma na kuandika.

Mara moja, mpango ulianza kuk-

INAENDELEA UK.12

# Ijue safari ya elimu nchini toka ‘Enzi za Mwalimu’ hadi iliko leo

INATOKA UK. 11

ishuhudiwa juhudi za kujenga shule nyingi za msingi hasa vijijini kupanua fursa hiyo kwa Watanzania wakati huo nchi ikiwa katika sura ya Muungano.

Serikali katika kuziba mapengo ya wataalamu kabla na baada ya mwaka huo mpango wa maendeleo, ilitumia marafiki wa nchi za Ulaya Mashariki na China zenye mtazamo kisiasa mlengo kushoto kama ilivyo itikadi za kijamaa nchini, kupata wataalamu.

Katika mwaka huo wa mpango mpya 1964, Chuo Kikuu cha Dar es Salaam kilitanuliwa na kuhamia iliko sasa Mlimani, kutoka katikati ya jiji Dar es Salaam ikimiliki vitivo vitatu; Sayansi, Sanaa na Sheria iliyoanza nayo.

Mwaka mmoja baadaye, 1965 katika jitihada za nchi kujitosheleza kitaalamu kwa fani za fedha, biashara na uongozi, kulianzishwa Chuo cha Elimu ya Biashara (CBE) jijini Dar e Salaam.

Pia mwishoni mwa miaka ya 1960 kulianza kushuhudiwa zaidi kundi la wahitimu wataalamu kutoka ughaibuni waliorejea baada ya masomo, wakibobea katika fani kama uhasibu, uhandisi mitambo ya nguo na udaktari binadamu. Ni fursa zilizokuwa endelevu kwa zaidi ya miaka 15.

**UPEPO WA 1970**

Huo ni mwaka ukibakia kipindi kidogo Rais Nyerere, alichowaahidi wakoloni ‘baada ya miaka 10 wafike kushuhudia...” Pia, serikali ilikuwa na nwaka mmoja tu tangu Mpango wa Maendeleo wa Pili (1969 - 1974) kuanza.

Katika historia ya elimu, 1970 katika lugha ya sasa mtaani ‘una jambo’ lake. Kwa makubwa ya sekta elimu. Hapo ndipo kuliundwa rasmi Chuo Kikuu cha Dar es Salaam, baada ya miaka 10 kuwa tawi la Afrika Mashariki, huku ikiendelea kubaki na mbia wake, Taasisi ya Elimu.

Pia ni mwaka wa kisheria Chuo Maendeleo ya Uongozi (IDM) Mzumbe kuzaliwa, ikiungana na CBE, UDSM na vingine vyenye historia kongwe kama vile Tengeru, Arusha kwa wataalamu wa ustawi wa jamii, vilevile Chuo cha Ufundi Dar es Salaam, maarufu Dar Tech, kikiwa endelevu katika uzalishaji mafundi.

Hadi kufika mwaka 1972, wanataaluma wengi kitaifa walisharejea nchini wahitimu wa mafunzo ya juu kihasibu, hasa ACCA na ACA ya Uingereza, kuziba pengo lililokuwapo nchini. Hapo serikali ilichukua hatua kupitisha sheria mbili kuu.

Ilianzishwa Bodi ya Taifa ya Uhasibu na Ukaguzi wa Hesabu (NBAA) kubeba dhamana kuu mbili; moja, msimamzi mkuu wa taaluma ya uhasibu nchini, pili kuratibu mitihani ya juu kwa vyeti viitwavyo CPA kwa maana aya ‘Certified Public Accountants’,

Kimsingi ni ngazi ya taaluma kama iivyo ACA na ACCA nchini Uingereza au RIA Canada, msamiati CPA ukitumika sana kwa nchi nyingi za Afrika chini ya Jumuiya ya Madola, mfano Kenya, Uganda na Zimbabwe.

Mwaka huo huo 1972, sekta ya fedha na fani jirani kama bima zilishuhudia neema ya kuanzishwa Chuo cha Usimamizi wa Fedha (IFM), Dar es Salaam, ambayo imedumu kuwa chimbuko la wahasibu nchini.

Kasi hiyo, pia ikaendelea shuleni hasa msingi kukiwapo msisitizo wa kipekee na mwaka 1973 serikali ilichukua hatua kama ya kuunda UDSM, ilipopitisha sheria ya kuundwa Baraza la Taifa la Mitihani na Elimu ya Ufundi (NACTE), kuondokana na mfumo tegemezi wa kusimamia mitihani nchini.

Hapo kukashuhudiwa mitaala na muhtasari wa masomo maarufu ya mwaka 1976, ikichukua mwelekeo mpya ulioboreshwa kitaaluma, pia ukibeba falsafa ya nchini na masmo kama vile Elimu ya Siasa, hadi katikati ya 1995 ikahamia Uraia.

Mwaka 1974, chama tawala wakati huo TANU, kilipitisha Azimio la Musoma kuhimiza Elimu kwa Wote, lililoamsha ushiriki kitaaluma kwa ngazi zote za kijamii katika sekta ya elimu kitaifa, wakiwamo wasiobahatika kuhudhuria shule.

Baada ya mwaka mmoja, 1975, Taasisi ya Elimu Tanzania ilihamishiwa katika Wizara ya Elimu na Utamaduni ikienguliwa kutoka kwa walezi wake, Kitivio cha Elimu cha Chuo Kikuu cha Dar es Salaam.

Baadaye, 1987 kisheria ilibadilishwa jina kutoka Taasisi ya Elimu hadi Taasisi ya Ukuzaji Mitaala, bila kubadilishwa jukumu ya msingi, kutokana na kujikita na ubunifu, pia kukuza mitaala ya ngazi mbalimbali za elimu.

**JICHO LA PEKEE**

Juhudi za Rais Nyerere, pia ilielekeza jicho la pekee katika namna ya kuwasaidia wasiobahatika kupata fursa ya elimu kutokana na madhila ya siasa zilizotangulia.

Mosi, katika kipindi chote cha uongozo wake Mwalimu Nyerere, mbali na kutoa elimu bure na huduma bora, sekta ya elimu ilipata fursa kubwa ikiwamo bajeti kubwa zaidi, hata kuna kipindi kufikia asilimia 25.

Nchini kukaanzishwa mfumo maalum wa elimu kuimarisha kusoma na kuandika uliokuwa na nafasi chini ya mpango wa pamoja na Umoja wa Mataifa kupitia chini ya Shirika la Elimu, Sayansi na Utamaduni (UNESCO).

Moja ya ajenda yake za msingi ikiwamo ya hivi karibuni UNESCO, ililenga watoto wote wenyewe umri wa kwenda shule wanufaishwe lengo kwa dunia litimizwe ifikapo mwaka 2015.

Kwa wakati huo nchini, kampeni ilitumika chini ya mkakati ulioitwa Mfumo wa Elimu kwa Wote (UPE). Hapo kutokana na siasa ya nchi, Ujamaa na Kujitegemea, umma wa wakazi mijini na vijijini walifundisha kwa kujitolea watu wazima ambao hawakupata nafasi hiyo.

Pia kutokana na pengo la walimu kuonekana, kulibuniwa mpango wa kuandaa walimu wa msingi zama hizo, wakichukuliwa wahitimu wa darasa la saba waliofanya vizuri wakapelekwa mafunzoni katika vyuo vya ualimu.

Hata walipohitimu na kuingia kazini walitaniwa kwa jina ‘Ualimu Pasipo Elimu’ kutokana msamiati UPE, ingawaje walikuwa na tija ya ngazi ya juu datrasani hata kuushangaza umma.

Ni kipindi madarasa ya UPE yalichachamaa kuibua wengi wasiojua kusoma na kuandika kwa kukosa fursa za zama hizo, sasa wakiwa na uelewa mkubwa. Ndio leo pameshuhudiwa baadhi yao wazee mahiri kusoma magazeti na mitandao ya simu.

Pia katika nafasi ya kujiunga darasa licha ya kuwapo juhudi kubwa tangu uhuru wa nchi bado nafasi hazikutosha, hata kuna baadhi ya walimu wakuu walipata mitihani ‘nani wa kumwandikisha na nani wa kumwacha.’

Ilichangia kubuniwa kipimo cha asili kilichopendwa, kumtathmini mtoto ukubwa wake kiumri kuanza shule, alitakiwa kunyoosha mkono wa upande mmoja mathalan kulia, aguse sikio la upande wa pili, kama kushoto.


Wakati huo umri wa kuanza darasa la kwanza ilikuwa miaka saba, tofauti na sasa miaka sita au pungufu na hakukuwapo ulazima kuanzia kisheria chekechea. Hadi sasa haijaachwa fikra hasi kwa vipindi vyote.

Hata hivyo, kuanzia awamu ya pili na zilizofuata (kabla ya awamu ya tano shuleni) mbali na mageuzi ya tija, ada ziliazishwa shuleni.

Kuliendelezwa kama Mpango wea Maendeleo Elimu (ERP) kwa awamu tofauti kuboreshwa elimu shuleni, chekechea lazima kwa watu wazima, Mpango Maalum wa Wasiojua Kusoma na Kuandika (MEMKWA) na hivi karibuni aliloamua kihistoria Rais Samia, waliopata ujauzito sasa kuendelea na elimu na wote waliochaguliwa vyuo vya elimu ya juu, wote wapatiwe mkopo.

Mengi yanayotekelezwa sasa, yana sura ya utekelezaji mipango ya maendeleo ya elimu nchini na mawazo yake yaliyodumu katika awamu nyingi uongozi wa nchi, 1964 ukiwa mwaka wa aina yake kutoa mwongozo.

Daima safari ya maendeleo nchini kitaifa haijawahi kupishana na elimu.



Wanafunzi wa Shule ya Sekondari Ihungo, Bukoba katika zama zao. Mmoja sasa ni mwanahabari mwandamizi na mwingine ofisa mwandamizi wa jeshi.




Jackson Makweta, mmoja wa mawaziri wakongwe walioweka rekodi katika utendaji wa Wizara ya Elimu. **PICHA ZOTE: MTANDAO**

ELIMU
NA MWANDISHI WETU

# WADAU: RUKSA KUREJEA SHULENI KUTAOKOA MAISHA MABINTI, 'VICHANGA'

## ▪Tusipojihadhari tutahuzunika- Daktari



Mwenyekiti wa Jukwaa la Vijana Kata ya Ulaya, Kilosa Pili Simba akizungumza na Nipashe.
**PICHA: MWANDISHI WETU**

MKULIMA anapoinama na kuanza kulima anainuka baada ya muda kuangalia ngwe yake, kutambua ukubwa au udogo wa kazi aliyoifanya na kujibu maswali mengi yanayoibuka anapotazama alipolima.

Leo Watanzania ni 'wakulima', wanatazama nyuma kujua ukubwa wa kazi iliyofanyika baada ya miaka 60 ya Uhuru wa taifa lao, uliopatikana Desemba 9, 1961.

Ngwe iliyolimwa ni kubwa na kazi iliyofanyika kuanzia Uhuru hadi leo inawafurahisha, wakiangalia nyuma kurejea tatizo la mabinti kupata mimba na kufukuzwa shule, walivunjika moyo.

Lakini leo kwenye jubilei ya miaka 60 ya uhuru kuwarejesha wasichana waliojifungua shuleni, kunawafurahisha, kunawagusa wengi wakiwamo wazazi, wauguzi, waganga na walezi.

Wapo wanaoipokea kwa mikono yote, kwa vile tangu uhuru mwanafunzi aliyepata mimba alikuwa mhanga tena si kwa kutumia sheria bali maamuzi yaliyorithiwa kutoka kwa mkoloni, kufukuzwa shule.

Kamati za Shule za Msingi na Bodi za Shule za Sekondari zilibariki kazi ya kuwafukuza wasichana shule wakati walimu wakuu wakikamilisha jukumu la kuwakabidhi kwa wazazi au walezi mabinti hao walionyimwa haki ya kusoma pengine kwa kubakwa na jamaa zao wa damu.

Hali ilikuwa mbaya kwa wasichana kwa sababu waliowapa mimba hawakuadhibiwa hadi mwaka 1998 ilipotungwa sheria ya makosa ya kujamiiana na kuharamisha ubakaji na kuwapa watoto mimba na aliyepatikana na hatia alitupwa gerezani miaka 30, hayo yakitokea baada ya miongo mitatu ya uhuru.

Mwezi uliopita serikali ikatangaza kuwarudisha shuleni wasichana baada ya kujifungua. Wadau wanapongeza hatua hiyo, wakieleza kuwa imeokoa maisha na kuwapa nafasi wale waliokuwa wasisome na kuelimika.

### KUOKOA MAISHA

Kufukuza wasichana shule kulisababisha wazazi, walezi, waliowapa mimba na mabinti waathirika kufikiria na kuamua kutoa mimba ikibidi kwa njia za kienyeji. Yote hayo yalisababisha vifo vya watoto na hata mama zao, lakini hilo sasa litapungua anasema Dk. Byabato Kamugisha, mhadhiri mstaafu wa vyuo vikuu.

Anampongeza Rais Samia Suluhu Hassan, kwa kuruhusu warudi shuleni kwa sababu maisha mengi yalipotea kutokana na wahusika kuharibu mimba kwa sababu ya kutaka watoto wao kuendelea na masomo na mabinti pia kutokuwa tayari kuwa na watoto.

Anasema hatua hiyo mbali na kupoteza maisha ili sababisha matatizo ya kiafya kwa baadhi.

Dokta Byabato anaongeza kuwa kitendo cha kuwazuia wasisome miaka ya nyuma kiliwakwamisha kimaisha watoto na wazazi hao wanafunzi kwa vile bila kusoma haikuwa rahisi kumudu maisha.

Anaeleza kuwa leo hii masuala ya lishe bora na afya ya malezi yanategemea elimu hivyo ni vyema kuwarudisha tena shuleni ili kuwawezesha kumudu maisha kwa vile wataelimika.

Aidha, anakumbusha kuwa mara nyingi kinamama ambao hawakusoma hata kwenye hatua za mwanzo inakuwa vigumu kusomesha watoto wao, hivyo kuwaruhusu kurudi darasani kumeongeza fursa zaidi kwao na watoto watakaowazaa kuendelea kusoma.

### SHERIA ISIMAMIWE ZAIDI

Kuruhusu wanafunzi kurudi shule kumeokoa maisha ya mama na watoto wao, ambao pengine wangeharibiwa kutokana na kuharibu mimba kienyeji.

Lakini, kuwarudisha mabinti shule hakutakuwa na tija kama sheria ya makosa ya kujamiiana haitasimamiwa kikamilifu na wahusika wa kuwapa mabinti mimba kusakwa, kushtakiwa na kuadhibiwa.

"Ni vyema kusimamia sheria ya watoto na ile ya makosa ya kujamiiana na kuwaadhibu wenye hatia. Lengo la kuwarudisha shuleni halitakuwa na tija kama mafataki, walaghai na wanaowarubuni watoto wataendelea na uhalifu." Anasema Catherine Salvatory, kutoka Chama cha Uzazi na Malezi Bora Tanzania (UMATI).

Anapohojiwa na Nipashe, anasema ni hatua kubwa na kazi ya kusaidia wasichana kurudi shuleni na kuendelea na masomo ni njema lakini bila kudhibiti unyanyasaji kingono, ubakaji kwa kusimamia sheria lengo halitatimia.

Catherine anasema: "Hatua hiyo ni nzuri lakini iende sambamba na kukomesha maeneo yanayochochea mimba mfano vibanda umiza, kuwa na madanguro yanayowatumikisha wasichana kingono, ukatili dhidi ya wasichana na kuwa mstari wa mbele kuwalinda watoto."

### WASICHANA MALENGO

Pili Simba ni Mwenyekiti wa Kikundi cha Vijana Tujitambue cha Kata ya Ulaya, kilichoko Kilosa Mkoa wa Morogoro, kinachohamasisha vijana kujitambua.

Anasema kuruhusu wasichana baada ya kujifungua kurudi shule ni jambo jema na kutaka waandaliwe na wawe na malengo.

Anawataka wasilichukulie poa warudi shuleni, lakini wafahamu kile wanachotaka ni kusoma au ni mambo mengine ya nje ya darasa?

"Ninasema hivi kwasababu wapo wanaobeba mimba kisa waache shule, hawa hawataki kusoma. Kama wamepewa nafasi wataendelea kubeba mimba kwa sababu hawataki shule? Ni jambo la kutafakari."

Anataka serikali ifahamu kuwa wapo waliopata mimba kwa kubakwa pengine hata na jamaa zao, hao kweli wanastahili kufikiriwa lakini wapo wasiotaka kusoma hawa wanatafuta mimba ili wasiendelee na masomo.

Pili anayefanyakazi na mashirika ya kuhamasisha vijana kujitambua na kupokea ujumbe wa afya ya uzazi salama na elimu ya ujinsia likiwamo UMATI, anasema ni lazima mabinti hao wahojiane, kushauriwa na kufanyiwa nasaha ili wawe na malengo na kupenda kusoma na kujiendeleza ili kuwabaini wale wasiotaka shule na kuwasaidia.

"Kuwaruhusu kurudi shuleni kwenda pamoja na kuchunguza sababu za ujauzito na iwapo msichana aliyeathirika anafurahia kusoma na pia kuwaelimisha wale wasiojua umuhimu wa kusoma," anashauri Pili.

### YAJAYO NI HUZUNI

Daktari Gloria Kunambi wa Kituo cha Afya Pugu Kajiungeni Dar es Salaam, anasema Tanzania inatakiwa kuwa na kampeni endelevu za kitaifa kuwakataza mabinti wasichezee viungo vya uzazi kwa vile miaka ijayo watakosa uzazi.

Anasema ambacho watu hawakijui ni hasara za mabinti kuanza ngono katika umri mdogo, kujiingiza kwenye mahusiano ambayo yanaharibu viungo vya uzazi na matokeo yake ni kukosa watoto miaka ijayo.

"Mimi ni mama na daktari ninachosema tunahitaji kampeni za kuwahimiza watoto wasifanye ngono utotoni siyo kuwafundisha masuala ya ujinsia na elimu ya uzazi salama. Tutakwama. Hatuwasaidii. Nchi inaweza kubaki ukiwa, ni muhimu kulinda viungo vya uzazi," anaonya Dk. Gloria.

Anapingana na hisia kuwa kuwaruhusu mabinti kurejea shule baada ya uzazi kutapunguza utoaji mimba, akisema hana uhakika na hilo na huenda ukaongezeka.

Serikali imeruhusu wasichana wanaopata mimba kujifungua na kuwanyonyesha watoto na kurudi shuleni baada ya miaka miwili na kuendelea na masomo.

TEKNOLOJIA

NA GAUDENSIA MNGUMI

# MSOMI: TUONGEZE NYUKLIA KWENYE KAPU LA NISHATI




Mitambo ya kurutubisha nyuklia barani Ulaya. **PICHA: MTANDAO**

KUNA msemo kuwa kwenye giza ni karakana ya shetani, ikimaanisha kuwa pasipo na nishati hufanyika kila aina ya uhalifu. Ni kwa ukweli huo kuwa taifa lisilo na mwangaza halina maendeleo.

Bila umeme elimu haitafanikiwa, shule za bweni zisizo na umeme zina uhalifu mwingi, mitaa isiyowaka umeme na taa usiku si salama, halikadhalika kazi za hospitalini bila umeme mchana na usiku hazifanyiki.

Ili Tanzania isiwe karakana ya ibilisi tangu Uhuru wa Tanganyika mwaka 1961 hadi sasa serikali imewekeza kwenye miradi mingi ya umeme.

Hata hivyo, Tanzania ya miaka 60 ya Uhuru inahitaji kuwa na umeme mwingi tena kutoka vyanzo mbalimbali si tu gesi wala maji au mafuta mazito kama ilivyo sasa, bali kuongeza vyanzo vingine vingi na vikubwa.

Ndivyo anavyosema Dk. Kamugisha Byabato, mhadhiri mstaafu wa vyuo vikuu katika mahojiano haya kuhusu miaka 60 ya Uhuru na uhakika wa nishati.

Dokta Byabato mtaalamu wa uhandisi madini na nishati jadidifu (mining engineering and renewable energy), anashauri.

Anasema Tanzania kwa namna yoyote ile ifikirie kuanzisha mradi wa umeme wa nyuklia bila kuhofia mtu wala taifa kwasababu nishati hiyo ndiyo ufunguo wa maendeleo ...anaendelea kusema:

**SWALI:** Tuambie Tanzania baada ya miaka 60 ya Uhuru kwenye eneo la nishati inatakiwa kufanya nini kuondokana na giza na kukatikakatika kwa umeme mara kwa mara?

**JIBU:** Inahitaji 'kapu kubwa la nishati' lenye umeme wa nyuklia, makaa ya mawe, jua (sola) gesi, upepo, joto ardhi (geothermal), maji na bayogesi.

Na kubwa zaidi ni kuchimba urani na kujenga vinu vya nyuklia na kuzalisha umeme wa uhakika. Kwa Tanzania urani inapatikana Namtumbo kwenye machimbo ya Mkuju, iko Bahi mkoani Dodoma, maeneo mengine ni pamoja na Manyoni, Songea, Tunduru, Madaba pamoja na Nachingwea.

Ziko kampuni zinachimba madini hayo na kuyasafirisha nje kwa ajili ya kuzalisha umeme, lakini taifa bado halijanufaika.

**SWALI:** Mara nyingi kuanzisha vinu vya kurutubisha nyuklia hasa kwa Afrika ili kuzalisha umeme vinapingwa na mataifa yaliyoendelea, unadhani itawezekana?

**JIBU:** Nchi ambazo zimetumia nyuklia na kuendelea kiuchumi zinazipinga nchi zinazoendelea zinapotaka kujenga miundombinu ya nishati ya nyuklia.

Mfano Korea Kaskazini imebanwa sana ili kuikwamisha kurutubisha nyuklia, lakini ufike wakati Tanzania na Afrika itumie yurani kuzalisha nishati.

Mataifa yote yaliyoendelea iwe Ulaya, Marekani na Japan, yamepata maendeleo haya kwa kutumia nishati ya nyuklia tangu miaka ya 1960. Maendeleo yaliyoko leo yameanzia kwenye kutumia umeme huo.

**SWALI:** Unadhani kuchimba na kutumia nyuklia kunavyopingwa na mataifa yaliyoendelea ikiwamo Ulaya kunaweza kufanyika kwa urahisi huku Afrika na Tanzania?

**JIBU:** Kuna kampuni ya Ufaransa ya AREVA hata leo inachimba urani nchini Niger Afrika Magharibi na inashughulika na uzalishaji wa nishati ya nyuklia, inashangaza kusikia kuwa nishati hiyo inapigwa vita duniani, si kweli.

AREVA na kampuni tanzu za SOMIR na COMINAK zote zinazochimba madini hayo kwa miaka mingi na nchi hiyo pamoja na mataifa mengine Ulaya yananufaika na madini hayo ambayo yanapatikana kwa wingi Niger .

Kwa hiyo siyo suala la kuendelea kufikiria kuwa vinu vya nyukilia vinapigwa vita Ulaya ni muda wa kuwekeza kwenye nishati ya nyuklia na kuacha kuruhusu madini yake kutumiwa bure na mataifa mengine wakati watu wake wanabaki gizani.

Kampuni za Ulaya zinachimba madini ya uranium Afrika na kuyachukua bure ili kuzalisha na kujihakikishia umeme wa kutosha kwa maendeleo yao, lakini kuwa na usalama wakati wa baridi kali ambayo ni changamoto kwa nchi nyingi za bara hilo.

Tukumbuke hakuna vita ya nyuklia vilivyowahi kupiganwa duniani mbali na mashambulizi yaliyofanywa na Marekani pekee nayo ni mabomu ya atomiki yaliyotupwa kwenye miji ya Japan ya Nagasaki na Hiroshima na Wamarekani wenyewe mwaka 1945 baada ya kumalizika Vita vya Pili vya Dunia.

> “Kampuni za Ulaya zinachimba madini ya uranium Afrika na kuyachukua bure ili kuzalisha na kujihakikishia umeme wa kutosha kwa maendeleo yao, lakini kuwa na usalama wakati wa baridi kali ambayo ni changamoto kwa nchi nyingi za bara hilo.

Hivyo inashangaza kuendelea kusikia eti mataifa yanakatazwa kutumia nyuklia kwa madai eti watarutubisha nyuklia na kuzalisha silaha. Zipi?

Wenzetu wanatukataza wanajua kuna kufanikiwa kwenye nyuklia. Ndiyo maana ninasema ni lazima tujitahidi kwa nguvu zote kuongeza nyuklia kwenye kapu la nishati zetu.

Ni nishati salama, kikubwa ni usalama kwa sababu ni madini yenye mionzi (radioactive materials) tuhakikishe mionzi inazuiliwa isiingie kwenye mazingira yetu na kuleta athari, lakini tujaribu kwa nguvu zote kuzalisha umeme huo.

**SWALI:** Nishati hii haiathiri jotoanga?

**JIBU:** Haina athari wala kuongeza joto duniani kama ilivyo kwa umeme wa visukuku (fossils) mfano gesi asilia, mafuta na makaa ya mawe

**SWALI:** Vipi kuhusu kutunza mabaki ya nyuklia, je, Tanzania itaweza kuyahifadhi yasilete athari kwa watu na mazingira?

**JIBU:** Hata nchi za Ulaya zinafanya utafiti wa utunzaji wa uchafu utokanao na uzalishaji wa nishati ya nyuklia. Kwa sasa uchafu wote unatunzwa kwenye matunzo ya muda. Ya kudumu hayajapatikana. Pia tukumbuke kuwa kama Ulaya hawatatunza mabaki hayo kikamilifu hata sisi ambao hatutumii umeme huo, tutadhurika. Ndiyo maana ni vyema na sisi tujiunge tuwe sehemu ya wanaotumia umeme huo.

**SWALI:** Unasema nishati yetu itoke kwenye vyanzo vingi kama makaa ya mawe, mbona duniani leo inasisitizwa kuachana umeme wa visukuku (fossils) mfano makaa ya mawe, unadhani Tanzania inaweza kutumia akiba ya makaa ya mawe yaliyoko Mchuchuma na Kiwira kuzalisha umeme?

**JIBU:** Kuna utaalamu wa kusafisha makaa ya mawe unaoitwa carbon sequestration na kuzuia hewa ukaa isiende angani na kuchafua angahewa na kuchangia kuongeza joto duniani. Hivyo kwa kutumia utaalamu na utafiti inawezekana kuzalisha na kutumia umeme wa makaa ya mawe.

Siyo hivyo tunahitaji kutumia umeme wa jua kwasababu Afrika ndilo bara pekee linalopata mwanga wa jua mwingi mno kuliko sehemu yoyote duniani.

Ni kwa sababu mistari yote mitatu ya kitropiki ya Kansa, Ikweta na Kaprikoni, inapita kwenye eneo hili lakini watu wake hawana umeme wa kutosha wa nishati jua.

Si hivyo tu hata nishati ya joto linalotokana na jua linalopatikana kwenye Jangwa la Sahara ni chanzo kingine kikuu cha umeme Afrika, hivyo wakati umefika wa kuamka na kuweka na si kuruhusu vyanzo vya nishati yake itumiwe kwa manufaa ya nchi nyingine.



# DC: Wenye ulemavu changamkieni mikopo

**Na Peter Mkwavila,** CHEMBA

MKUU wa Wilaya ya Chemba, Simon Chacha, amewataka watu wenye ulemavu kuchangamkia fursa za mikopo ya asilimia mbili inayotolewa na halmashauri.

Aidha, amewataka kuzitumia fedha hizo kwa malengo ya kuinua biashara zao badala ya kuzipeleka katika shughuli za anasa na kushindwa kurejesha madeni ya mikopo hiyo kwa wakati.

Chacha alibainisha hayo juzi kwenye maadhimisho ya Siku ya Kimataifa ya Watu wenye Ulemavu iliyofanyika kimkoa wilayani hapa.

Akizungumza kwa niaba ya Mkuu wa Mkoa wa Dodoma, Athony Mtaka, alisema serikali kupitia halmashauri zake zinatoa mikopo kwa makundi mbalimbali ikiwamo ya vijana, wanawake na watu wenye ulemavu.

Hivyo aliwataka walemavu kuhakikisha kuwa wanachangamkia fursa hiyo ya mikopo ambayo inauwezo wa kuwaondolea maumivu ya kiuchumi.

"Ninawaomba ndugu zangu watu wenye ulemavu mchangamkie fursa hiyo ya mikopo ya asilimia mbili ambazo zinazotolewa na halmashauri ili muweze kujikomboa kwenye suala zima la uchumi," alisema Chacha.

Pia, aliwataka wazazi na walezi kuacha tabia ya kuwaficha ndani watu wenye ulemavu kwa kuwa kitendo hicho ni ukatili, unyanyapaa na unyanyasaji.

Alisema, bado kuna changamoto baadhi ya wazazi na walezi wamekuwa wakiwaficha watu wenye ulemavu, suala ambalo linakuwa gumu hata kwa serikali kufahamu takwimu sahihi ya walemavu.

Awali Katibu wa shirikisho la vyama vya watu wenye ulemavu (SHIVYAWATA) mkoa wa Dodoma, Justus Ng'wantalima, alisema kuwa uelewa mdogo juu ya ukopaji mikopo ya asilimia mbili kwa watu wenye ulemavu bado ni changamoto kwa walio wengi.

Katibu huyo alisema bado kundi la watu wenye ulemavu wanahitaji elimu ya kutosha kwa ajili ya kuchangamkia fursa mbalimbali zinazotolewa na serikali ikiwamo mikopo.

"Bado kuna umuhimu mkubwa kwa serikali kupitia watendaji wake wa halmashauri kutoa elimu zaidi ili watu wenye ulemavu waweze kuchangamikia hii mikopo iliyopo kwa ajili yao,"alisema.

Hata hivyo, aliiomba serikali kuanzia ngazi ya vitongoji, vijiji hadi kata kuwashirikisha watu wenye ulemavu ili na wao waweze kushiriki katika kutoa maamuzi kwenye vikao vinavyohusu maendeleo.

# Viongozi wa dini waombwa hamasa ya chanjo corona

**Na Peter Mkwavila,** DODOMA

WAKATI likiibuka wimbi la nne la corona, viongozi wa dini wameshauriwa kuhamasisha waumini wao kujitokeza kupata chanjo inayotolewa bure kwenye vituo mbalimbali vya huduma.

Aidha, viongozi hao wameshauriwa kuhamasisha waumini wao kuzingatia maelekezo ya Wizara ya Afya ikiwamo uvaaji wa barakoa kunawa mikono kwa maji tiririka na sabuni na kutumia vipukusi.

Ushauri huo ulitolewa na Mwenyekiti wa Jumuiya ya Maridhiano mkoa wa Dodoma, Askofu Dk. Evance Chande, alipokuwa akizungumza na waandishi wa habari jijini Dodoma kuhusu tishio la mlipuko wa virusi hivyo.

Dk. Chande alisema viongozi wa dini wanao wajibu mkubwa katika kuhakikisha wanaisaidia serikali kupitia Wizara ya Afya kutoa elimu ya kujilinda na ugonjwa wa Uviko-19.

Alisema, elimu hiyo ni pamoja na ile ya kuwafundisha waumini kuepuka mikusanyiko isiyo ya lazima ikiwamo ni pamoja na kuratibu ibada ambazo zitazingatia maelekezo ya Wizara ya Afya.

"Viongozi wa dini tuendelee kuwahamasisha waumini wetu kama ilivyokuwa kawaida yetu, ili waendele kufuatilia na kuzingatia taarifa ya wimbi hili la nne kutoka Wizara ya Afya ambako ni chanzo sahihi katika kutoa taarifa nchini,"alisema.

Hata hivyo, mwenyekiti huyo aliwaomba viongozi hao wa dini kwa kupitia maeneo yao ya ibada kuwatoa hofu waumini wao na kuwaasa kuendelea na shughuli za kujiingizia kipato huku wakizingatia maelekezo kutoka wizara ya afya.

Mwenyekiti huyo pia alipongeza wizara hiyo ya afya kwa kuwapatia Watanzania takwimu za UVIKO -19 ikiwamo tahadhari juu ya ujio wa wimbi la nne katika taifa.

"Kwa kweli jambo hili litakuwa msaada mkubwa kwa sisi viongozi wa dini kuingia upya kwenye maombi huku tukizingatia ushauri kutoka wizara yetu hii ya afya," alisema.

Hivi karibuni, Wizara ya Afya ilitoa taarifa kuwa kuna ugunduzi mpya wa kirusi anayetambulika kwa jina la Omicron (B.1.1529) taarifa kutoka Shirika la Afya Duniani (WHO).



Mwenyekiti wa Jumuiya ya Maridhiano Mkoa wa Dodoma, Askofu Dk. Avance Chande, akiwaongoza waumini wa dini mbalimbali kuliombea taifa, huku wakishikilia bendera ya taifa ikiwa ishara ya kumwomba Mungu awaepushie Watanzania kirusi kipya kilichoibuka cha ugonjwa wa Uviko-19 kwenye ibada iliyofanyika Kanisa la EAGT Ipagala mkoani Dodoma, jana. **PICHA: PETER MKWAVILA**

# Wazazi watajwa chanzo mimba za utotoni

**Na Paul Mabeja,** DODOMA

TAMAA ya mali kwa wazazi wilayani Chamwino, imetajwa kuwa moja ya sababu inayochangia vitendo vya ukatili wa kijinsia ikiwamo ndoa za utotoni na mimba katika umri mdogo kwa watoto wa kike.

Hayo yalibainisha juzi na baadhi ya wazazi walipokuwa wakichangia mjadala uliofanyika katika kijiji cha Manchali, kuhusu vitendo vya ukatili wa kijinsia wilayani humo katika maadhimisho ya Siku 16 za Kupinga Ukatili wa Kijinsia.

Magreth Lengai, alisema bado lipo tatizo kubwa la mimba za utotoni na ndoa za utotoni wilayani hapo ambalo kwa kiasi kikubwa linachangiwa kwa asilimia kubwa na wazazi.

"Wazazi wanashawishi watoto kupata mimba katika umri mdogo na kuwaozesha hii yote ni kutokana na tamaa za mali na mtoto anafundishwa na mazazi kuwa asimtaje aliyempatia ujauzito lakini baada ya muda wanafungishwa ndoa," alisema.

Alisema sababu nyingine ya watoto kupata mimba katika umri mdogo ni umbali wa shule hali inayowalazimu kutembea umbali mrefu kila siku na kukumbana na vishawishi njiani.

Kutokana na hali hiyo, aliiomba serikali kuwekeza kwenye ujenzi wa mabweni kwa ajili ya kuwahudumia watoto wa kike ili watimize ndoto zao.

"Watoto wa kike wanapokwenda shule kila siku asubuhi na kurudi jioni wakati mwingine wanapewa lifti za magari na kwenye hizo lifti yapo mambo mbalimbali yanaendelea unakuja kushtuka tuu mtoto anajauzito,"alisema.

Aidha, alisema wazazi wamekuwa wakishirikiana na watoto wa kike kuwafundisha kuwa wasifanye vizuri kwenye mitihani yao ya mwisho ili waoelewe kwa kisingizio cha kutokuwa na fedha.

Robert Songo, alisema hivi sasa wilayani humo kuwekuwapo na matukio mengi ya wazazi kuozesha watoto wao katika umri mdogo kuanzia miaka 14.

"Nimewahi kushuhudia jamaa anaozesha mtoto wa miaka 14 na hii ni kutokana na tamaa ya mali na umaskini uliopo hivyo mtu nafanya mtoto kama bidhaa ya kujipatia fedha,"alisema.

Mchungaji Emmanuel Mdabwa wa Parishi ya Manchali, alisema amekuwa akipokea watoto wengi wa umri chini ya miaka 18, ambao wanaletwa na wazazi wao kuja kuandikisha ndoa.

"Kuna wakati wazazi walileta mtoto wa miaka 14 wanataka nimfungishe ndoa, lakini mtoto yule tayari aliyashakuwa mjamazito nikawafukuza,"alisema Mchungaji Mdabwa.

Lucy Mpali, alisema pamoja na uwepo wa matukio hayo ya mimba za utotoni lakini bado ukatili wa kijinsia wa ukeketaji kwa watoto wadogo unaendelea kufanyika.

"Hivi sasa wazazi wamekuwa wajanja sana mtoto akizaliwa tuu wanamfanyia ukeketaji kwa kufikicha ile sehemu ya siri kwa kutumia tumbaku pamoja na vitu vingine wanavyo vijua wao,"alisema Mpali.

Kadhalika, alisema katika ukeketaji huo kinamama ndiyo watu wa kulaumiwa kwani wamekuwa wakifanya matukio hayo kimyakimya bila waume zao kujua chochote.

"Kuna wakati fulani watoto walifanyiwa ukeketaji wakawa wamewekwa ndani kama wagonjwa wa kawaida, lakini wakazidiwa ikabidi waitwe madakatari kwenda kuwasaidia watoto wale kabla hawajapoteza maisha,"alisema Mpali.





# Wamachinga waomba kuboreshewa eneo jipya

**Na Nebart Msokwa,** MBEYA

WAFANYABIASHARA wadogo maarufu Machinga waliohamishiwa katika eneo la Uwanja wa Ndege wa zamani jijini Mbeya, wameiomba serikali kuwaboreshea mazingira.

Baadhi ya mambo waliyoombwa waboreshewe ni mitaro ya maji ili wasidhurike na mafuriko.

Wakizungumza na Nipashe juzi wajasiriamali hao walisema walihamishwa na halmashauri kwenye maeneo yao ya awali ikiwamo maeneo ya Kabwe na Mwanjelwa wakapelekwa kwenye eneo hilo bila kuwa na maandalizi mazuri.

Joshua Daimon alisema serikali imewagawia maeneo ya kufanyia shughuli zao, lakini hakuna mitaro ya uhakika ya kuondoa maji na hivyo wanapata hofu ya maji kuanza kutwama katika eneo hilo.

Alisema kwa sasa mvua bado haijaanza kunyesha hivyo wanafanya biashara vizuri, lakini ikianza wana wasiwasi kwamba eneo hilo litakuwa halipitiki kirahisi.

"Serikali imetuleta hapa na imeamua daladala ziwe zinapita huku ili tupate wateja jambo ambalo ni zuri, lakini sasa tatizo lipo kwenye miundombinu maana hili eneo ni bonde linalopokea maji," alisema Joshua.

Naye Sifa Mwalimbe alisema eneo hilo likitwamisha maji wateja hawatakuwa wanaingia na badala yake watakuwa wanahamia kwenye masoko mengine jambo ambalo litawasababishia kukosa wateja.

Alisema eneo hilo ni zuri kwa biashara lakini linatakiwa kuboreshwa kwa kuwekewa miundombinu ya maji ili yasitwame na kusababisha matope ambayo yataathiri kazi zao.

Alisema eneo hilo waliombewa na Mbunge wa Jimbo la Mbeya Mjini, Dk. Tulia Ackson, kwa aliyekuwa Rais wa awamu ya Tano, Hayati Dk. John Magufuli ambaye alikubali na kuagiza maeneo hayo kuwekewa miundombinu.




Kaimu Mganga Mkuu wa Mkoa wa Mbeya, Dk. Osmunda Mwanyika (katikati), akipokea msaada wa dawa za uzazi wa mpango kutoka kwa mabalozi wa T- MARC Tanzania, Dk. Isaac Maro (kushoto) na Dk. Romana Malikusema, jijini Mbeya mwishoni mwa wiki. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# Corona yatajwa kikwazo ajira duniani

**Na Nebart Msokwa,** MBEYA

MLIPUKO wa virusi vya corona duniani umetajwa kuwa chanzo kikuu cha tatizo la ajira duniani, ambapo inadaiwa asilimia 81 ya waajiriwa wote duniani wameathirika.

Aidha, mabadiliko ya sayansi na teknolojia yametajwa kuwa chanzo kingine cha kupungua kwa ajira duniani kwa maelezo kuwa kwa sasa kazi nyingi zilizokuwa zinatakiwa kufanywa na binadamu zinafanywa na mashine inayoendeshwa na mtu mmoja.

Hayo yalisemwa na Mwenyekiti wa Baraza la Chuo Kikuu cha Mzumbe, Pius Maneno wakati wa mahafali ya 20 ya Chuo hicho Ndaki ya Mbeya ambapo alisema virusi vya corona vimesababisha shughuli za uzalishaji kupungua.

Alisema baadhi ya shughuli za uzalishaji zimefungwa kutokana na mitaji kupungua na kwamba baadhi ya wawekezaji wamepunguza kiwango cha fedha kwenye shughuli zao na hivyo kupunguza mahitaji ya wafanyakazi na mishahara.

Maneno alisema ili kukabiliana na tatizo la Virusi vya corona kila Mtanzania anatakiwa kuchukua tahadhari zinazoshauriwa na wataalamu na kwamba hata serikali inatakiwa iendelee kuhimiza wananchi kuchukua tahadhari.

"Lakini tunaiomba serikali ibadili mwelekeo kwa kuwekeza zaidi kwenye teknolojia ili tuendane na mapinduzi ya nne ya viwanda duniani, sasa hivi shughuli nyingi zinafanywa na mashine," alisema Maneno. Mlau wa Chuo cha Mzumbe, Prof. Cyprius Binamungu, alisema tatizo la corona lilivuruga hata mfumo wa ufundishaji vyuoni kwa madai kuwa wahadhiri na wanafunzi walikuwa wanaogopana kila upande ukiogopa kuambukizwa.

Alisema wanafunzi walikuwa wanawaogopa wahadhiri na wahadhiri walikuwa wanawaogopa wanafunzi na kwamba wakati mwingine walilazimika kuanza kufundisha kwa njia ya masafa.

Alisema tatizo lilikuwa kubwa zaidi pale ambapo mmoja wao alikuwa na tatizo la kupiga chafya ama kukohoa jambo ambalo lilikuwa linazua hofu miongoni mwao wakiamini kuwa anayefanya hivyo alikuwa na maambukizi ya corona.

Alisema pamoja na mazingira hayo, bado wahadhiri waliendelea kuingia madarasani na wanafunzi wakaendelea kusoma kwa bidii mpaka wakafanikiwa kuhitimu.

"Kutokana na mazingira mliopitia, nawashauri sana mjitahidi sana kwenda kufanya kazi kwa nguvu, maarifa na weledi ili kufikia malengo yenu," alisema Prof. Binamungu.

Kwa upande wake Makamu Mkuu wa Chuo Kikuu cha Mzumbe, Prof. Lughano Kusiluka, alisema chuo hicho kinafanya utafiti maalumu wa kubaini endapo maarifa wanayotoa kwa wanafunzi yanaendana na mahitaji ya soko.

Alisema utafiti huo wanawashirikisha wahitimu wa chuo hicho katika kipindi cha miaka mitatu, waajiri wao pamoja na wafanyakazi wenzao ambao wameajiriwa kwenye taasisi tofauti ndani na nje ya nchi. Alisema endapo watabaini kuwa stadi wanazowafundisha wanafunzi haziendani na mahitaji ya soko watabadili na kuanza kutoa mafunzo yanayoendana na soko hilo.

Vilevile alisema chuo hicho kinatekeleza miradi 19 ya utafiti na kwamba chuo hicho kinakabiliwa na tatizo la uhaba wa baadhi ya miundombinu ya ufundishaji.

## Wadau wa tumbaku waombwa kuchangia ujenzi shule ya wasichana

**Na Nebart Msokwa,** CHUNYA

MKUU wa Mkoa wa Mbeya, Juma Homera, amevitaka vyama vya msingi vya wakulima wa tumbaku, kampuni za ununuzi wa zao hilo pamoja na wadau wengine wa zao hilo kuchangia fedha kwa ajili ya ujenzi wa shule ya wasichana ambayo itasaidia kupunguza mimba kwa wanafunzi.

Homera alitoa agizo hilo alipofanya ziara ya kukagua maendeleo ya kilimo cha zao hilo katika Kata ya Lupa ikiwa ni pamoja na kutembelea vitalu vya miche ya miti inayotarajiwa kupandwa na wakulima kwa ajili ya kupunguza uharibifu wa mazingira unaosababishwa na kilimo hicho.

Alisema shule hiyo itajengwa katika Kata ya Lupatingatinga, lakini itachua wanafunzi wa kike kutoka katika maeneo yote ya wilaya hiyo na kwamba shule hiyo itakuwa ya bweni.

Aliagiza vyama vyote vya Msingi vya Wilaya hiyo kuchangia Sh. 500,000 kila kimoja, makandarasi wanaoandaa miche ya miti kila mmoja kuchangia Sh. milioni mbili kwa ajili ya mradi huo huku akiwaagiza viongozi wa Kata ya Lupa kutafuta eneo kwa ajili ya mradi huo.

Vilevile alizuia fedha zote ambazo vyama hivyo vya msingi vya wakulima wa tumbaku vilikuwa vinachangia kwenye Chama cha Maendeleo ya Elimu Chunya (CHUDET) kupelekwa kwenye chama hicho na badala yake zipelekwe kwenye mradi huo wa shule.

"Tunataka watoto wetu hawa wasome katika mazingira mazuri, hatutaki watembee muda mrefu kwenda shuleni, tunataka tupunguze mimba kwa wanafunzi wetu, nataka shule hii iwe ya kisasa na iwe ya mfano," alisema Homera.

Alisema ili kuweka usawa Halmashauri ya Wilaya hiyo inatakiwa kuandaa utaratibu wa kuwashirikisha wachimbaji wa madini katika Wilaya hiyo kujenga Shule ya Msingi ya Mchepuo wa Kiingereza.

Mkuu wa Wilaya ya Chunya, Mayeka Simon Mayeka, alisema kwa sasa wanaendelea na mazungumzo na wachimbaji wa madini wilayani humo ili na wao wachangie kwenye ujenzi wa miradi mbalimbali ya elimu na afya.

Alisema wilaya hiyo imegawanyika katika kanda kuu mbili ambazo ni ukanda wa madini ya dhahabu na ukanda wa kilimo hasa cha tumbaku ambalo ndilo zao kuu la biashara kwa wilaya hiyo.

Mayeka alisema wilaya hiyo imekuwa ikikabiliwa na tatizo la mimba kwa wanafunzi kutokana na sababu mbalimbali hali ambayo inahitaji nguvu za wadau pamoja na serikali kukomesha vitendo hivyo.

"Hivi tunavyozungumza kuna kesi moja hivi ya mwanafunzi kuozwa katika wilaya hii, nawaombeni sana wakulima tushirikiane katika jambo hili ili tumalize tatizo hili, Mkuu wetu wa Mkoa ametuanzishia jambo zuri sana," alisema Mayeka.

Kwa upande wake Mwenyekiti wa Halmashauri ya Wilaya ya Chunya, Bosco Mwanginde, alisema halmashauri yake pia itachangia kwenye ujenzi huo ili kuhakikisha tatizo la mimba kwa wanafunzi linakuwa historia.



# Tume kupunguza maambukizi VVU

**Na Rahma Suleiman,** ZANZIBAR

MWENYEKITI wa Bodi ya Tume ya Kupambana na Ukimwi Zanzibar, Dk. Salhiya Muhsin, amesema wamejipanga kuhakikisha kwamba wanapambana na makundi hatarishi ambayo yamekuwa yakiongezeka katika maambukizi ya Virusi vya Ukimwi.

Miongoni mwa makundi hayo ni watu wanaojidunga na sindano wanaotumia dawa za kulevya ambayo ni asilimia 48.

Dk. Muhsin aliyasema hayo jana Mjini Zanzibar wakati akitoa taarifa za mikakati ya Tume ambayo imejipanga ifikapo mwaka 2030 kuhakikisha maambukizi ya ugonjwa huo kwa makundi hatarishi yanapungua kwa kiwango kikubwa.

Aliyataja makundi ambayo hatari yanayochangia kuongezeka kwa ugonjwa wa Ukimwi ni wanaume wanaofanya mapenzi ya jinsia moja yamefikia asilimia 60, huku wanawake wanaojiuza miili yao kwa kufanya mapenzi yapo kwa asilimia 73.

"Tumejipanga kutoa elimu kuhusu ugonjwa wa Ukimwi na athari zake kwa ujumla katika makundi ya vijana wanaojidunga sindano ambao ni wale wanaotumiya madawa ya kulevya kwa asilimia 45," alisema.

Aidha, alisema maambukizi ya ugonjwa huo yamekuwa yakipungua ambapo katika mwaka 2010 jumla ya kesi 366 zimeripotiwa, huku maambukizi yakishuka na kufikia 177 katika mwaka 2020.

Naye Mwakilishi wa Shirika la Kimataifa linaloshughulikia mapambano ya Ukimwi (UNAID), Gorge Loy, alisema wamejipanga kuongeza nguvu zaidi katika mapambano dhidi ya Ukimwi ikiwamo kutoa elimu ya ugonjwa huo kwa makundi ya rika mbalimbali likiwamo la vijana.

Mkuu wa Mkoa wa Kusini Unguja, Rashid Hadiid Rashid, amesema wamejipanga kupambana na kupunguza kasi ya ugonjwa huo ikiwamo maambukizi mapya zaidi baada ya kubainika kwamba Wilaya ya Kati ndiyo eneo ambalo lipo katika hatari ya vijana kuambukizwa na ugonjwa huo.

**"Tumejipanga kutoa elimu kuhusu ugonjwa wa Ukimwi na athari zake kwa ujumla katika makundi ya vijana wanaojidunga sindano ambao ni wale wanaotumiya madawa ya kulevya kwa asilimia 45," alisema.**

# Waziri: Wazazi, walezi toeni ushirikiano vita ya udhalilishaji

**Na Rahma Suleiman,** ZANZIBAR

WAZIRI wa Afya na Ustawi wa Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto, Nassor Ahmed Mazrui, amewataka wazazi na walezi kushirikiana na serikali katika mapambano ya vitendo vya udhalilishaji wa kijinsia dhidi ya wanawake na watoto.

Aliyasema hayo Mjini Zanzibar baada ya makabidhiano ya vifaa vya matumizi mbalimbali kwa ajili ya nyumba salama ya kuhifadhia waathirika wa udhalilishaji vilivyotolewa na Mwakilishi Mkaazi wa Shirika la Umoja wa Mataifa la Uhamiaji (IOM) nchini, Dk. Qasim Sufi.

Alisema vitendo vya udhalilishaji ni janga la kitaifa hivyo iko haja jamii kushirikiana kwa pamoja na serikali ili kuhakikisha vitendo hivyo vinaondoka katika jamii.

Aidha, aliitaka jamii kutokuwa na muhali wa kuwaficha wahalifu wa vitendo hivyo kusaidia mapambano ya vita dhidi ya udhalilishaji.

"Ni wajibu wetu kushirikiana kwa pamoja kuunga mkono mapambano ya vita dhidi ya udhalilishaji wa wanawake na watoto tuacheni muhali, tuwe mstari wa mbele kwa kutoa ushahidi wa ukweli," alisema waziri.

Naye Dk. Sufi alisema iko haja kusaidia nyumba salama Zanzibar kwa lengo la kukabiliana na vitendo vya udhalilishaji.

Alisema tatizo hilo ni la kidunia ambalo likiwaathiri husussan wanawake na watoto ambao wameonyesha kuathirika zaidi duniani kote.

Mkurugenzi wa Idara ya Ustawi wa Jamii na Wazee, Abdalla Saleh Omar, alisema nyumba salama inapokea watoto waliofikwa na kadhia mbalimbali ikiwamo udhalilishaji wa kingono kama kubakwa, kulawitiwa na kupigwa kupitiliza.

Pia alisema usafirishaji haramu wa waathirika ambao hutumika kwa kufanyakazi za majumbani wakiwa katika umri mdogo hupatiwa hifadhi ya muda watoto hao, ambapo kwa kipindi cha Agosti hadi Oktoba mwaka huu, waathirika waliopokelewa 22 katika nyumba salama kwa hifadhi ya muda.

Hata hivyo, alisema waathirika hao wa kike ni 19 na wa kiume watatu na kwamba wengine hupelekwa katika nyumba salama kwa hofu ya kudhurika ikiwa wazazi wakishtukiwa kuwa watumiaji wa dawa za kulevya pamoja na watoto waliokosa ndugu na jamaa.



Siti Juma akiwa katika maonyesho ya Siku ya Mji Mkongwe ambayo yalifanyika mwishoni mwa wiki huko Forodhani Zanzibar, akiwa na bidhaa mbalimbali za zamani ambazo zilitumika kwa familia za Kizanzibari. **PICHA: RAHMA SULEIMAN**

# RC awataka Wingwi kupeleka watoto shule

**Na Rahma Suleiman,** ZANZIBAR

MKUU wa Mkoa wa Kaskazini Pemba, Salama Mbarouk Khatib, amewataka wazazi wa kijiji cha Wingwi kuwapeleka watoto wao shule na kuacha kuwaingiza katika ajira mbaya, hivyo kukosa elimu.

Alisema hayo jana alipotembelea wananchi wa vijiji vya Wingwi na Tumbe ambapo alihamasisha wazazi kuwapeleka watoto wao shule.

Alisema serikali ya Zanzibar inatekeleza mradi wa kuwarudisha shule watoto waliotoroka na kujiingiza katika ajira ngumu, hivyo kukosa fursa ya elimu.

Alisema Wilaya ya Micheweni Pemba ni eneo ambalo limeathirika kwa watoto kuacha shule na kujiingiza katika kazi za uvuvi na kugonga kokoto.

"Serikali ya Mkoa wa Kaskazini Pemba tunatekeleza mradi mkubwa wa kuwarudisha shule watoto waliotoroka kuanzia umri wa mwaka 7 hadi 15, ambapo tunahitaji ushirikiano mkubwa na wazazi ambao ndiyo wanaoishi na watoto hao," alisema.

Naye Mkuu wa Wilaya ya Micheweni Pemba, Mgeni Khatib, alisema tumefanikiwa kuwarudisha baadhi ya watoto waliotoroka shule katika mradi wa kuwarudisha shule watoto waliokimbia ambao unafadhiliwa na Shirika la EAC la Qatar.

Alikiri Wilaya ya Micheweni kuathirika na tatizo la watoto wengi kuacha shule na kujiingiza katika ajira ngumu ambazo hawastahiki kuzifanya, huku kisingizio kikubwa kikiwa ni hali ngumu ya maisha.

Mwalimu Haji Ali Hamadi wa Shule ya Tumbe, alisema wamefanikiwa kuwarudisha watoto 58 pamoja na kutenga madarasa mawili kwa ajili ya kupokea wanafunzi hao.

# MATANGAZO MCHANGANYIKO

## KUPOTEA KWA PASIPOTI YA KUSAFIRIA



**RASHID JUNIOR HILAL** anatangaza kupotelewa na hati ya kusafiria (PASIPOTI) yenye namba za usajili TAE412438, yeyote atakayeiokota atoe taarifa kituo chochocte cha polisi

Polisi taarifa **MAG/RB/3568/2021**

116602502

## KUPOTEA KWA KADI YA PIKIPIKI

**IBRAHIM OMARI NASSORO**

Anatangaza kupotelewa kwa kadi ya pikipiki (haojue) gs group limited yenye namba za usajili **MC 685 BLS** yeyote atakae iyona atoe taarifa kituo cha polisi au piga simu namba **0623780765**

**MOR /MOR/RB/5717700/2021**

116602202

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**

**BARAZA LA ARDHI NA NYUMBA-MWANZA**

**SHAURI NO. 107 YA 2021.**

**JEREMIAH JOHN MAHALU……………………… MDAI**

**DHIDI YA**

1. **AZANIA BANK LIMITED**
2. **DAVID CHIGULU …………………… WADAIWA**

**WITO WA KUITWA MAHAKAMANI**

**KWA: DAVID CHIGULU**

Unafahamishwa kwamba Mleta maombi hapo juu amefungua Shauri/Ombi dhidi yako katika Baraza la Ardhi na Nyumba Mkoa wa Mwanza, ombi hili limepangwa kutajwa tarehe 15/12/2021 katika Chumba cha Baraza, Jengo liko Mkabala na Mahakama ya Mwanzo mjini na Mahakama ya wilaya ya Nyamagana.

Kwa hiyo unatakiwa kuhudhuria katika Baraza siku hiyo wewe mwenyewe, wakili wako au mtu mwingine anaye ruhusiwa kisheria kujibu ombi hilo.

KAA- Ukija kwamba kushindwa kufika, Baraza litasikiliza ombi hilo na kutoa uamuzi bila wewe kuwepo.

Imetolewa nami kwa Amri na Chapa ya Baraza leo tarehe 29/11/2021

MURIRYA N. MWENYEKITI BARAZA LA ARDHI NA NYUMBA MWANZA

116602102

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**MAHAKAMA YA TANZANIA**

**Katika Mahakama ya mwanzo ya Wilaya ya ………..…TANGA**

**Kituo cha…………MJINI TANGA……. Mkoa………TANGA**

**Usimamizi wa Mirathi…………17…………2021**

**KATIKA SHAURI LA MIRATHI YA MAREHEMU…… HUSSEIN ADAM KAROTA…….**

**KATIKA SHAURI LA MAOMBI YA KUMTEUA MSIMAMIZI YALIYOLETWA**

**NA….ADAMU HUSSEIN KAROTA….**

**TANGAZO**

**(Kanuni ya 5(2) ya Kanuni za Usimamizi wa Mirathi Mahakama za Mwanzo)**

Watu wote wanaodai kuwa na uhusiano wowote/maslahi yeyote na mirathi ya marehemu tajwa hapo juu, wanaalikwa kuja kuhudhuria katika shauri hili endapo wakitaka kufanya hivyo mnamo tarehe 27/12/2021 kabla huyo mwombaji hajateuliwa kuwa msimamizi wa mirathi hiyo.

Wosia wa marehemu huyo upo mahakamani waweza kukaguliwa. Tarehe 6/12/2021

HAKIMU MKAZI MAHAKAMA YA MWANZO TANGA MJINI

116602702

**JAMHURI YA MUUGANO WA TANZANIA**

**HATI YA KUITWA SHAURINI MDAIWA (MCA/63)**

**MAHAKAMA YA MWANZO YA BUKOBA MJINI, WILAYA YA BUKOBA**

**MADAI YA TARAKA NAMBA 24 YA 2021**

**Mdai……. VEDASTO CHRISTOPHER FELICIAN**

**Anamdai**

**Mdaiwa……ADELAIDA S. VALENCY**

**Kwa ADELAIDA S. VALENCY**

Kwa kuwa Mdai/Wadai ameleta/ wameleta madai yake/yao ya talaka, kwa hiyo unahitajika/mnahitajika kuhudhuria binafsi katika mahakama hii siku ya ALHAMIS tarehe 16/12/2021 saa 2:30 asubuhi kwa kujibu madai hayo na kwa kuwa siku hiyo ni siku ya kukatwa shauri hilo, ni lazima kuleta mashahidi wako/wenu na hati zote zinazohusu shauri hilo kwa ajili ya kujitetea katika shauri hilo.

Angalia kama hukuhudhuria/ hamkuhudhuria siku iliyotajwa hapo juu, mahakama ikithibitisha kama umepokea/ mmepokea kuitwa shaurini, itaweza kutoa maamuzi kuwa umeshindwa/ mmeshindwa.

Kuitwa shaurini kumetolewa kwa maombi ya VEDASTO CHRISTOPHER FELICIAN.

Hati hii imetolewa kwa amri yangu na chapa ya mahakama hii leo tarehe 6/12/2021.

116602802

## KUPOTEA KWA KADI YA GARI

Ndugu **EDDI ABDALLAH MALIKI** anatangaza kupotelewa na kadi ya gari aina ya **TOYOTA DYNA** yenye namba za usajiri **T 399 AVA.** Chassis namba **BU30088776** Engine namba **B0517622** Kwa yeyote atakayeiona atoe taarifa kituo chochote cha Polisi kilicho karibu.

Taarifa Polisi:

**KOR/RB/6163/2020**

116602002

## KUPOTEA KWA KADI YA GARI

**WILFRED JUSTINE MOLEL**

ANATANGAZA KUPOTEA KWA KADI YA GARI YENYE NO YA USAJILI **T167ACY** JINA LA KADI PHIBE KAITIRA MURUSURI CHASSIS NO **SXA110222018** ENGINE NO **3S2649855** ATAKAYEIONA ATOE TAARIFA KITUO CHA POLISI

**ARU/ARU/RB/539322/2021**

116601902

## KUPOTEA KWA KADI YA GARI

**PETER LUCAS CHAMI.**

Anatangaza kupotelewa na kadi ya gari yenye namba za usajili **T.479 BUB,** aina ya NOAH, yenye Chassis **No.SR400167385,** Engine No. **3S5114320.**

Yeyote atakayeiona atoe taarifa kituo cha polisi kilichopo jirani yake,

Taarifa ya jeshi la polisi,

**KAH/RB/TR/605/2021.**

116601802

## KUPOTEA KWA KADI YA BAJAJ

**GROLI YAHANES MADUKE**

anatangaza kupotelewa na kadi ya **BAJAJ** yenye namba za usajili **MC 244 BZJ** Mali ya cheses namba **MD2A21BY5JWA87249** injini namba **PFZWJA76502** Kwa yeyote atakayeiona atoe taarifa polisi

Taarifa ya polisi RB. Namba

**IRI/IRI/RB/568303/2021**

116601702

**IN THE COURT OF DISTRICT DELEGATE OF MOROGORO**
**DISTRICT AT MOROGORO**

**PROBATE AND ADMINISTRATION**

**CAUSE NO 65 OF 2021**

**In the Matter of the Estate of the Late MARTINA YOVIN MKAMBA**

**By 1. MACMILLAN DAVID MKAMBA**
**2. …………………………………………….**

All persons claiming to have any interest in the estate of the above named deceased are hereby cited to come and see the proceedings if they think fit before the grant of probate (or letter of administration) is made to the above –named petitioner.

Objection to the grant should be filed on or before the 04 day of JAN….. 2022

Dated at MOROGORO this **03day of DEC………2021**

RESIDENT MAGISTRATE

116601602

## KUPOTEA KWA CHETI



**ABDALLAH HARUNA MPULILA** anatangaza kupotelewa na cheti cha kidato cha nne chenye index namba **S2316/0007** kilichotolewa na baraza la mitihiani kupitia shule ya secondary ya BUHINGU mwaka 2016, yeyote atakayekiokota atoe taarifa kituo chochote cha polisi.Polisi taarifa **MOR/MVO/RB/536025/2021**

116601302

## KUPOTEA KWA KADI YA GARI

**FELIX PAULO LYIMO**

anatangaza kupotelewa na kadi ya gari aina ya **TOYOTA HARRIER** yenye namba za usajili **T 383 DHW,** yeyote atakayeiokota atoe taarifa kituo chochote cha polisi

Polisi taarifa

**KMR/RB/9185/2021**

116601202

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**MAHAKAMA YA TANZANIA**

**Katika Mahakama ya Mwanzo Kihonda**
**Wilaya ya Morogoro, Mkoa wa Morogoro**

**Usimamizi wa Mirathi na 05 2021**

**KATIKA SHAURI LA MIRATHI YA**

**MAREHEM: Habibu Omari Kisako WA Morogoro Mjini**
**KATIKA SHAURI LA MAOMBI YA KUMTEUA MSIMAMIZI YALIYOLETWA NA MOSHI HABIBU LUGELO**

**TANGAZO**

**(kanuni ya 5(2)ya kanuni za usimamizi wa Mirathi Mahakama za Mwanzo)**

Watu wote wanaodai kuwa na uhusiano wowote/maslahi yoyote na mirathi ya marehemu tajwa hapo juu,wanaalikwa kuja kuhudhuria katika shaurini hili endapo wakitaka kufanya hivyo mnamo tarehe 07/12/2021 kabla huyo mwombaji hajateuliwa kuwa msimamizi wa Mirathi hiyo.

Endapo kuna yoyote mwenye wosia na marehem anaweza kuuleta mahakamani kukaguliwa.

- Wosia wa marehemu huyo upo Mahakamani waweza kukagulia.
- Marehem hakuacha wosia
- Futa isiyo husika

Imetolewa Tarehe 26/11/2021

116601502

**Uza,**

**Chenye Thamani Kubwa Kwa**

**Kutangaza Nasi Kwa Bei Poa**

**Tupigie 0782253676**

**OFISI ZA MATANGAZO**

**Mikocheni Industial Area,**

**Po.Box 31042, Dar es Salaam. Mob: +255 - 745 700 710.**

**E-mail: advertise@guardian.co.tz, website: www.ippmedia.com**

TAHADHARI: Wasomaji wanatakiwa kuuliza na kuchukua ushauri sahihi kabla ya kutuma fedha, au kuingia katika gharama yoyote kati yake na mtangazaji THE GUARDIAN LIMITED hawatahusika kwa malipo au manunuzi yoyote kati ya muuzaji na mnunuaji kwa matangazo yaliyochapishwa katika gazeti hili.

## HABARI KITAIFA

# Wahasibu wafundwa utunzaji wa mazingira

**Na Mwandishi Wetu**

KAMPUNI ya ulinzi ya SGA imetoa msaada wa miti kwa ukumbi wa mikutano wa APC ulioko Bunju Dar es Salaam na kuwafunda wahasibu namna ya utunzaji wa mazingira kwa kupanda miti.

Akizungumza katika mkutano wa mwaka wa wahasibu uliofanyika katika ukumbi huo wa APC, Mkurugenzi Mtendaji wa SGA Tanzania, CPA Eric Sambu, ambaye alikuwa mmoja wa watoa mada katika mkutano huo, alitoa wito kwa wahasibu nchini kujenga utamaduni wa kupanda miti katika kila tukio au sherehe.

Aliwahamasisha kuhusu uharibifu wa mazingira unaosababishwa na ukataji wa miti huku akisisitiza kuwa kukata miti bila kuotesha mingine ina maana ukanda wote unaweza kugeuka kuwa jangwa kwa hivyo ni muhimu kila mmoja achukue jukumu la kuotesha miti na kuhamasisha jamii pia kuotesha miti kwa wingi.

"Kama kampuni inayotoa huduma za usalama na ulinzi, tunaamini utunzaji wa mazingira ni mwanzo wa maisha bora na hili lilisisitizwa katika mkutano wa COP 26 uliofanyika Scotland," alisema.


## NOTISI YA KULIPA DENI NA TANGAZO LA MNADA WA HADHARA

Kampuni ya **MASE INTERNATIONAL LIMITED, JOSINA COMPANY LIMITED & AUCTIONEER, LOCUS DEBT MANAGEMET LTD NA MAK RECOVERIES LTD** Kwa idhini tuliyopewa na **FINCA MICROFINANCE BANK LTD** tunatoa muda wa siku 14 kwa wadaiwa walioorodheshwa kwenye jedwali hapo chini wawe wamelipa madeni wanayodaiwa na **FINCA MICROFINANCE BANK LTD.** Kinyume na hapo tutalazimika kuuza kwa njia ya mnada wa hadhara mali walizoweka kama dhamana ya mkopo. Tarehe za kufanya minada zitatolewa kwa njia ya vipeperushi na magari ya matangazo kwenye sehemu dhamana zilipo.

| NOTISI KULIPA DENI NA TANGAZO LA MNADA WA HADHARA | | | |
|---|---|---|---|
| | MASE INTERNATIONAL LIMITED | | |
| S/N | JINA LA MDAIWA | AINA YA DHAMANA | MAHALI ILIPO DHAMANA |
| 1 | PAUL K NGANDAWAZA | NYUMBA YENYE MKATABA WA MAUZIANO | MTAKUJA-KATORO-GEITA |
| 2 | SIMON M LUMEREZI | NYUMBA YENYE MKATABA WA MAUZIANO | MCHONGOMANI-KATORO |
| 3 | MADUHU N NYAGA | NYUMBA YENYE MKATABA WA MAUZIANO | IBISABAGENI-SENGEREMA |
| 4 | KISIRI R MHOCHI | NYUMBA YENYE MKATABA WA MAUZIANO | MBUGANI-GEITA |
| 5 | ALIWAKILI M SAMSON | NYUMBA YENYE MKATABA WA MAUZIANO | NYANTOROTORO-GEITA |
| 6 | COSMAS A ABDALLAH | NYUMBA YENYE MKATABA WA MAUZIANO | NYANKUMBU-GEITA |
| 7 | TOLLAH M SHADRACK | NYUMBA YENYE HATI MILIKI KIWANJA NA.107 A (HD) SAFU "MW" NA NYUMBA YENYE HATI MILIKI KIWANJA NA 1B(HD) SAFU H | MWABARUHI NA IBISABAGENI-SENGEREMA |
| 8 | TWALIBU HUSSEIN FUND | BAJAJI YENYE NAMBA ZA USAJILI MC 708 BWX | GEITA TOWN |
| 9 | JOSEPH JAMES MKAMA | NYUMBA YENYE MKATABA WA MAUZIANO | KATORO |
| | JOSINA COMPANY LIMITED AND AUCTIONEER | | |
| 10 | EDWIN N. KAENA | NYUMBA YENYE MKATABA WA MAUZIANO | IZIGO-BUKOBA . |
| 11 | KAMGISHA R. DANIEL | NYUMBA YENYE MKATABA WA MAUZIANO | RWAMISHENYI-BUKOBA |
| | LOCUS DEBT MANAGEMENT LTD | | |
| 12 | RIZIKI S MGAYA | KIWANJA CHENYE HATI MILIKI KIWANJA NA 54 .KITALU M CHENYE MAJINA RIZIKI SIPULI MGAYA KILICHOPO NJOOS "A"NA NYUMBA MDHAMINI YENYE LESENI YA MAKAZI YENYE MAJINA MERCY CHAULA ILIYOPO MGENDELA NJOMBE. | NJOSS"A" NA MGENDELA-NJOMBE |
| 13 | OSCAR JOHN DANDA | NYUMBA YENYE LESENI YA MAKAZI NA. NTC 12657 | KAMBARAGE-NJOMBE |
| 14 | ROSE J MAYEMBA | GARI AINA YA RV4 TOYOTA YENYE NA.T604AYJ NA TOYOTA RAV4 YENYE NA.235 CND | MAGODA-NJOMBE |
| 15 | EDWIN S KIVALE | NYUMBA YENYE LESENI YA MAKAZI NA,1001 | MAGEGELE-MAKAMBAKO |
| 16 | WINFRED D KYANDO | KIWANJA CHENYE MKATABA WA MAUZIANO | UWEMBA IKISA-NJOMBE |
| 17 | GODLOVE JOSEPH MWALONGO | KIWANJA CHENYE LESNI YA MAKAZI NA, 4767 | MGENDELA-NJOMBE |
| 18 | SHUKURU MGATA | NYUMBA YENYE MKATABA WA MAUZIANO | IPOGOLO-IRINGA |
| 19 | NORBERTH S. SUMKA | NYUMBA YENYE MKATABA WA MAUZIANO | MKWAWA-IRINGA |
| 20 | SHEDRACK J. MUKUTA | KIWANJA CHENYE MKATABA WA MAUZIANO | IKUVILO-IRINGA |
| 21 | ISSACK REWARD NYUNZA | KIWANJA CHENYE MKATABA WA MAUZIANO | MAWELEWELE-IRINGA |
| 22 | MARTIN JOHN MNKAI | NYUMBA YENYE MKATABA WA MAUZIANO | MTIVILA-IRINGA |
| 23 | MOSHI D NGWAULANGA | NYUMBA YENYE MKATABA WA MAUZIANO | MAWELEWELE-IRINGA |
| | MAK RECOVERIES LTD | | |
| 24 | ABDURAHAMAN A ZAYUMBA | GARI AINA YA TOYOTA LAND CRUISER YENYE NA,ZA USAJILI T 116 ACY | KOROGWE-TANGA |
| 25 | AMINA H MKANGA | GARI AINA TOYOTA PASSO YENEYE NA. ZA USAJILI T 123 DCY | TANGA MJINI |

**MASHARTI YA MNADA**

1. Ukaguzi unaruhusiwa kuanzia tarehe ya tangazo hili.
2. Dhamana itauzwa kama ilivyo.
3. Mnunuzi atayeshinda anapaswa kulipa 25% ya bei aliyofikiwa siku ya mnada, na 75% iliyosalia atalipa ndani ya siku kumi na nne (14) toka tarehe ya mnada, Kinyume na hapo kiasi kilichotolewa awali hakitarudishwa na mnada utarudiwa tena.
4. Gharama zozote ikiwemo kubadilisha Hati miliki (transfer of ownership), na kumtoa mtu kwenye nyumba/eneo lililouzwa ni la mnunuzi.
5. Mnada utafanyika mahali ambapo dhamana zilipo na si vinginevyo.

KWA MAWASILIANO ZAIDI PIGA NAMBA

Mkurugenzi Mtendaji
Mase International Limited
S.L.P 6197 Mwanza
Namba Za simu: 0743 885084/0710885084

Mkurugenzi Mtendaji.
Josina Company Limited and Auctioneer
S.L.P 40855 MWANZA
NAMBA ZA SIMU; 0713203040/ 0768203040

NA
Mkurugenzi Mtendaji,
Locus Debt Management Ltd
S.L.P 4110 Dar es Salaam
NAMBA ZA SIMU: 0756140199/0716790393

Mkurugenzi Mtendaji,
Mak Recoveries Ltd
S.L.P
Dar es Salaam

NAMBA ZA SIMU; 0783224965/0715375475
Na
Finca Microfinance Bank Ltd
P.O. Box 78783
Mobile#: 0768790399, 0754774949

116603102



## BODI YA MICHEZO YA KUBAHATISHA TANZANIA

GAMING BOARD OF TANZANIA

## TAARIFA KWA UMMA

### UFAFANUZI JUU YA MKANGANYIKO WA USIMAMIZI NA UTOAJI WA LESENI ZA KUENDESHA MICHEZO YA KUBAHATISHA NCHINI

**Bodi ya Michezo ya Kubahatisha Tanzania (GBT)** imebaini uwepo wa ukiukwaji wa taratibu za utoaji LESENI/VIBALI vya kuendesha biashara za michezo ya kubahatisha nchini na hivyo kusababisha mkanganyiko kwa waendeshaji. Hivi karibuni baadhi ya mamlaka zingine za Serikali zimekuwa zikijihusisha na utoaji leseni/vibali vya kuendesha biashara za michezo ya kubahatisha kinyume na Sheria ya Michezo ya Kubahatisha Na. 4 ya mwaka 2003 (Gaming Act No. 4 of 2003) inayosimamia uendeshaji wa michezo ya kubahatisha hapa Tanzania.

**Tunapenda kuufahamisha umma kuwa leseni/vibali vya kuendesha biashara za michezo ya kubahatisha hapa nchini hutolewa na Bodi ya Michezo ya Kubahatisha Tanzania peke yake. Hii ni kufuatia Marekebisho ya Sheria ya Leseni Na. 25 ya Mwaka 1972 (Business Licensing Act No. 25 of 1972) yaliyofanyika mwaka 2003, kupitia Sheria ya Fedha Na. 15 ya Mwaka 2003 (Finance Act No. 15 of 2003) kifungu cha 5(1) (f), kuondoa michezo ya kubahatisha katika orodha ya shughuli za kibiashara zinazohitaji aina zingine za leseni za biashara, isipokuwa leseni inayotolewa na GBT tu.**

***Ifahamike kuwa, leseni za kuendesha biashara za michezo ya kubahatisha hutolewa baada ya mwombaji kukidhi vigezo vilivyoainishwa katika Sheria inayosimamia uendeshaji wa michezo hii nchini na si vinginevyo. Vigezo hivyo ni pamoja na muombaji kufanyiwa upekuzi wa kina (background check).***

Hivyo, lengo la taarifa hii ni **kuondoa mkanganyiko unaojitokeza mara kwa mara kati ya waendeshaji na baadhi ya maafisa biashara, maafisa utamaduni na maafisa polisi katika maeneo mbalimbali nchini.** Mkanganyiko huu kwa kiasi kikubwa unaathiri uendeshaji na usimamizi wa sekta ya michezo ya kubahatisha nchini kwa kuleta usumbufu kwa waendeshaji na hivyo kuikosesha Serikali mapato. Matumaini yetu ni kuwa **Taarifa hii itaondoa Mkanganyiko uliojitokeza** na kuiwezesha sekta ya michezo ya kubahatisha kuendelea kuchangia mapato ya Serikali na kulijenga Taifa letu ipasavyo.

***Kwa maelezo au maswali yoyote kuhusiana na usimamizi wa uendeshaji wa Michezo ya Kubahatisha nchini, tafadhali wasiliana nasi kupitia anuani hapo chini.***

Imetolewa na

**Mkurugenzi Mkuu**
**Bodi ya Michezo ya Kubahatisha Tanzania**
**Mtaa wa Mission/Sokoine Drive,**
**Ghorofa ya 27, PSSSF Twin Towers, Wing 'A'**
**S. L. P. 1717 Dar Es Salaam, Simu: 022 2124703/4/0800 1100 51**
**Barua pepe: info@gamingboard.go.tz**
**Tovuti: www.gamingboard.go.tz**

216602602

# KIRENGO FC MABINGWA UMOJA CUP 2021 RORYA

**Na Mwandishi Wetu, RORYA**

MICHUANO ya Umoja Cup 2021 iliyokuwa ikiendelea wilayani Rorya, imemalizika kwa Kirengo FC kutangazwa mabingwa baada ya kuibuka na ushindi wa mikwaju ya penalti 4-3 dhidi ya Wanamaji FC kwenye mchezo mkali wa fainali uliopigwa mwishoni mwa wiki katika Uwanja wa Maji Sota wilayani humo.

Katika mchezo huo, dakika 90 zilimalizika kwa sare tasa, ndipo Mwamuzi Amady Augustino, alipoamuru changamoto ya mikwaju ya penalti kuchukua nafasi yake kwa mujibu wa kanuni za michuano hiyo na Kirengo kuibuka washindi.

Wanamaji FC wangeweza kuibuka kidedea mapema tu katika dakika ya tatu, lakini bao lao lilikataliwa na mshika kibendera, Francis Azaria akidai mfungaji alikuwa ameotea kabla ya kuukwamisha mpira nyavuni.

Akizungumzia bao hilo, Kocha wa Wanamaji, Godfrey Josepha, alimtupia lawama mshika kibendera, Azaria kwa kukataa bao lao ambalo kwa maoni yake lilikuwa halali huku akiweka wazi kuwa hatakubali siku nyingine mechi yao kuchezesha na mwamuzi, Augustino.

"Goli letu lilikuwa halali kabisa, hatutegemei kuchezeshwa na mwamuzi huyu tena [Amady Augustino], mshika kibendera alitunyang'anya tu bao letu," alisema Josepha.

Kwa ushindi huo, mbali na kombe, Kirengo FC imezawadiwa Sh. 350,000 huku Wanamaji pia wakipata kombe kama mshindi wa pili sambamba na Sh. 250,000, timu iliyoshika nafasi ya tatu Mennonite FC, ambayo Ijumaa iliibuka ushindi wa mabao 5-2 ndidi ya Shirati Mji kwenye mechi ya kutafuta mshindi wa tatu, imezawadiwa Sh. 150,000.

Kwa upande wa Mchezaji Bora wa michuano hiyo, Riziki Abega wa Wanamaji FC na Mfungaji Bora, Nikolas Antony kutoka Kirengo FC aliyemaliza na mabao sita, kila mmoja alizawadiwa Sh. 25,000. Mbali na zawadi hizo kwa washindi, pia waandaaji wa michuano hiyo walitoa pole kwa familia ya Abega, ambaye alifariki dunia hivi karibuni pamoja na ngao ya heshima kwa Mzee Owino Jami, mmoja wa wazee waliopo mstari wa mbele katika kuendeleza soka Rorya.

Akizungumza wakati wa kukabidhi zawadi kwa washindi, mgeni rasmi katika fainali hiyo, Ofisa Michezo wa Wilaya ya Rorya, Charles Masanja, ambaye alimwakilisha mkuu wa wilaya hiyo, alitoa pongezi kwa waandaji wa michuano hiyo huku akimwomba mdhamini wa mashindano hayo, Peter Owino, kupanua wigo zaidi wa michezo wilayani humo.

Kwa upande wa mdhamini, Owino ambaye amekuwa akidhamini michuano hiyo kwa mwaka wa tisa sasa, alihimiza umoja na ushirikiano ndani ya Rorya na kuwapa pole Wanamaji FC kwa kupoteza fainali ya tatu mfululizo.

"Tumelipokea ombi la DC [mkuu wa wilaya] kupitia kwa ofisa michezo, hivyo kwa kushirikiana na ofisi yake tutapokea maelekezo katika kuendeleza michezo wilayani kwetu ili Rorya iende sambamba na maelekezo ya kitaifa ya sera ya michezo," alisema Owino.




Ofisa Michezo wa Wilaya ya Rorya, Charles Masanja (kushoto) na Mdhamini Mkuu wa Michuano ya Umoja Cup, Peter Owino (katikati), wakikabidhi kombe na cheti cha ushiriki kwa Nahodha wa Kirengo FC, Anthony Okea, baada ya timu yake kuibuka mabingwa kwenye mechi ya fainali dhidi ya Wanamaji FC juzi katika Uwanja wa Maji Sota, Rorya. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# Samia Taifa Cup kunguruma Dar Ijumaa

**Na Saada Akida**

MKURUGENZI wa Idara ya Maendeleo ya Michezo Wizara ya Utamaduni, Sanaa na Michezo, Yusuph Singo, amesema maandalizi ya mashindano ya Samia Taifa Cup yamekamilika huku yakitarajiwa kuanza kutimua vumbi Ijumaa wiki hii hadi Desemba 16, mwaka huu, Dar es Salaam.

Akizungumza na waandishi wa habari jijini jana, Singo alisema mikoa 31 tayari imethibitisha kushiriki kutoka Tanzania Bara na Zanzibar huku timu zikitarajiwa kuwasili kesho na keshokutwa.

Alisema katika mashindano hayo, michezo itakayoshindaniwa ni mitatu ambayo ni soka, riadha mbio fupi kwa wanaume na wanawake pamoja na mchezo wa netiboli na kwamba tayari Kagera wamethibitisha kushiriki katika michezo miwili, netiboli na riadha.

"Kwa upande wa Dar es Salaam inashiriki mkoa mmoja na mashindano hayo yatakuwa katika makundi, timu itakayofungwa katika hatua hiyo haitakuwa imeaga michuano hiyo," alisema Singo.

Alisema malengo makubwa ya mashindano hayo ni kuhakikisha wanatoa fursa kwa vijana kuonyesha vipaji vyao na kupata nafasi ya kuonekana na klabu mbalimbali ili kusajiliwa.

"Tuna tarajia hii michuano itafungua milango kwa vijana kuonyesha kiwango chao na kupata fursa ya kuonekana na kuajiriwa, tunatambua michezo ni ajira kwa sasa," alisema Singo.

Alisema kwa sasa wanaanza na michezo hiyo na ana matumaini baada ya hapo wataboresha kwa miaka mingine kuongeza idadi ya michezo ambayo haijawekwa katika mashindano hayo.

## Harmonize, Stamina kukiwasha Ijumaa

**Na Faustine Feliciane**

WASANII Harmonize 'Konde Boy' na Stamina, ni miongoni mwa mastaa watakaotoa burudani kwenye tamasha la wanafunzi wa vyuo vikuu la 'Freshers Bash' litakalofanyika Ijumaa wiki hii kwenye viwanja vya Posta, Dar es Salaam.

Tamasha hilo limeandaliwa na Jumuiya ya Wanafunzi, Taasisi ya Elimu ya Juu Tanzania (TAHLISO), lengo likiwa ni kuwakutanisha wanafunzi wa vyuo vikuu pamoja.

Akizungumza na waandishi wa habari jana, Makamu Mwenyekiti wa TAHLISO Taifa, Hijja Milambo, alisema mbali na wasanii hao pia Linah Sanga, Young Lunya na Dullah Makabila nao watatoa burudani.

"Kutakuwa na shughuli mbalimbali zitakazokuwa zikifanyika kwenye tamasha, wanavyuo watapata fursa ya kukutana na kubadilishana mawazo, lakini kutakuwa na viongozi na watu maarufu," alisema Milambo.

Alisema tamasha hilo licha ya kuandaliwa kwa ajili ya wanafunzi, lakini mtu yeyote anaruhusiwa kushiriki na kupata burudani kutoka kwa wasanii hao huku kiingilio kikiwa ni Sh.10,000 tu.

## Malindi mambo bado magumu Ligi Kuu Z'bar

**Na Hawa Abdallah, ZANZIBAR**

TIMU ya soka ya Malindi imeendelea kuzikosa alama tatu katika mechi tatu mfululizo baada ya juzi kulazimishwa sare ya mabao 2-2 dhidi ya KMKM katika mchezo wa Ligi Kuu Zanzibar inayodhaminiwa na Benki ya Watu wa Zanzibar, PBZ.

Malindi ambayo ilianza vizuri katika mzunguko wa kwanza hadi wa saba, majonzi yalianza kuiandama kuanzia raundi ya nane na tisa kwa kukubali vichapo kabla ya jana kugawana alama na wapinzani wao baada ya kuambulia sare.

Kwa matokeo hayo, Malindi sasa imefikisha alama 18, huku KMKM ikiwa na pointi 22 baada ya timu zote kushuka dimbani mara 10 katika ligi hiyo inayoshirikisha miamba 16 msimu huu.

Akizungumza na gazeti hili jana, Kocha Mkuu wa KMKM, Ame Msimu, alisema timu yake inaendelea kupambana ili ifanye vizuri zaidi licha ya kupata sare tatu katika michezo kumi.

"Tumeanza vizuri, na tupo vizuri, mapungufu ya kiubinadamu ni kawaida kutokea kwa wachezaji, inategemea na bahati utakayoshuka nayo uwanjani, hivyo tunazidi kujiimarisha kwa mbinu na uchezaji," alisema.

## ZISIKUPITE

### TOURE AKARIBISHWA ARSENAL

KOCHA wa Arsenal, Mikel Arteta amesema yupo tayari kusaidiana na mchezaji wa zamani wa Manchester City raia wa Ivory Coast, Yaya Toure kuinoa timu hiyo. ***(Sunday Mirror)***

### SALAH ASUBIRIA MKATABA

MSHAMBULIAJI wa Liverpool, Mohamed Salah, mwenye umri wa miaka 29, amerejea tena kauli yake kwamba, anataka kuendelea kubaki katika klabu hiyo lakini "uamuzi uko mikononi mwa utawala wa klabu na ni lazima watatue suala hilo". Mkataba wa mshambuliaji huyo Mmisri unamalizika katika msimu wa majira ya joto mwaka 2023. ***(MBC Masr TV, via Liverpool Echo)***

### RUIZ ATAKIWA LIVERPOOL

MCHEZAJI wa kimataifa wa Hispania, Fabian Ruiz analegwa na Liverpool, ambao wanataka kumwingiza kikosini kiungo huyo wa kati wa Napoli mwenye umri wa miaka 25 msimu ujao. ***(Fichajes.net)***

### HAG YUPO TAYARI UNITED

KOCHA wa Ajax, Erik ten Hag, amehusishwa na taarifa za kuchukua ukocha kule Manchester United na Mholanzi huyo amesema yuko tayari. ***(De Volkskrant, via Mirror)***

### DEMBELE APEWA MUDA

BARCELONA watamwomba winga Mfaransa, Ousmane Dembele kuwaambia iwapo atasaini nao mkataba mpya kufikia Desemba 31, mwaka huu, huku mkataba na mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 24 ukitarajiwa kumalizika msimu huu. ***(Sport)***

### MERTENS ATAKA MKATABA

MSHAMBULIAJI Mbelgiji Dries Mertens, amesema ana matumaini Napoli watachagua kurefusha mkataba wake. Mkataba wa sasa wa mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 34, unatarajia kumalizika mwishoni mwa msimu huu. ***(Sky Sports Italia)***

### MBAPPE HAJAAMUA

MSHAMBULIAJI wa Ufaransa, Kylian Mbappe, hajaamua iwapo hatoendelea kucheza Paris St-Germain, ambao walikataa ofa kutoka Real Madrid kwa ajili ya mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 22 kipindi cha majira ya joto. Mkataba wa Mbappe na PSG unamalizika msimu huu. ***(Amazon Prime, via Goal)***

### CABALLERRO NA SOUTHAMPTON

KLABU ya Southampton itaangalia uwezekano wa kumsajili golikipa wa Argentina Willy Caballero, ambaye ni mchezaji huru baada ya kuondoka Chelsea mwishoni mwa msimu uliopita. ***(Talksport)***

### FERNANDEZ ANUKIA LEEDS

LEEDS United wamekubali dili la Espanyol katika kumsajili mshambuliaji Mateo Joseph Fernandez mwenye umri wa miaka 18. ***(Mail on Sunday)***

### ELYOUNOUSSI HAONDOKI

WINGA wa Southampton na Norway, Mohamed Elyounoussi mwenye umri wa miaka 27, ambaye amekuwa akihusishwa na Arsenal na Leicester City, amesema kuwa familia yake sasa imetulia katika klabu hiyo. ***(Hampshire Live)***

# DONDOO ZA SOKA MAGAZETI YA ULAYA




# MBAPPE AELEZA KUUMIA KUTOJIUNGA REAL MADRID

## Kukatishwa tamaa kwa kushindwa kuondoka? Si kidogo, nilikuwa nakwenda kucheza klabu kubwa...

**PARIS, Ufaransa**

NYOTA wa Paris Saint-Germain, Kylian Mbappe amebainisha kwamba, "alikatishwa tamaa" kwa kutojiunga na miamba ya Ligi Kuu Hispania, LaLiga, Real Madrid kipindi cha majira ya joto kilichopita.

Huku mkataba wake ukiwa unamalizika mwishoni mwa msimu huu wa 2021-22, Mbappe alikuwa akihusishwa sana na mpango wa kuondoka PSG kwenda Madrid, ambao hawajaficha siri namna wanavyovutiwa naye.

Hata hivyo, uhamisho huo haukufanikiwa wakati PSG - bado ikiwa na nia ya kumpa mkataba mpya nyota huyo wa Ufaransa ambaye aliukataa.

Madrid inatarajia kumsajili Mbappe kama mchezaji huru mwishoni mwa msimu huu, lakini mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 22, aliulizwa kuhusu kushindikana kwake kwenda kule Santiago Bernabeu.

"Kukatishwa tamaa kwa kushindwa kuondoka? Si kidogo," alisema Mbappe akiiambia Amazon wakati akizungumza na gwiji wa Ufaransa, Thierry Henry.

"Si rahisi, lakini chochote kilichotokea, nilikuwa nakwenda kucheza kwenye klabu kubwa. Mimi ni mtu wa Paris, nahisi vizuri tu, lakini nilitaka kupata kitu kingine kabisa."

Uvumi ulianza kuenea kuhusu majaliwa ya Mbappe baada ya Euro 2020, wakati mshambuliaji huyo alipokosa penalti na Ufaransa kushindwa kufuzu hatua ya 16-bora dhidi ya Uswisi.

Mbappe hakufunga kwenye Euro na alitoa asisti moja wakati mabingwa hao wa dunia wakitolewa.

Mbappe, ambaye alijiunga na PSG akitokea kwa wapinzani wao, Monaco awali kwa mkopo mwaka 2017, ameshinda mataji matatu ya Ligue 1 na klabu hiyo.

MECHI KALI
HOME
AWAY
RB LEIPZIG
3.24 | 3.77 | 2.06
MANCHESTER CITY
CHEZA USHINDE JACKPOT TZS. 761
KUWEKA PESA:
- PIGA *150*87#, CHAGUA 4
- WEKA PESA.
tigo pesa vodacom m-pesa halopesa airtel money EZYPESA
SEND
SportPesa
SPORTPESA.CO.TZ
PIGA *150*87#
GBT:0249 HUDUMA KWA WATEJA MASAA 24, PIGA:
18+ 0764115588, 0677115588
0685115588
@TZSportPesa @SportPesaTZ @tzsportpesa

# RANGNICK AMPIGIA SALUTI FRED



**MANCHESTER, England**

KOCHA wa Manchester United, RALF Rangnick, amemsifia Fred kwa kuonyesha kiwango bora wakati ikipata ushindi wa kwanza chini ya kocha huyo wa muda, kwenye mchezo wa Ligi Kuu England, juzi.

Shuti la dakika ya 77 la nyota huyo wa kimataifa wa Brazil, liliiwezesha Man United kupata ushindi wa bao 1-0 dhidi ya Crystal Palace wakati Rangnick akiiongoza timu hiyo kwa mara ya kwanza.

Bosi huyo wa zamani wa Hoffenheim na RB Leipzig, alikuwa jukwaani wakati United ikiibuka na ushindi wa mabao 3-2 dhidi ya Arsenal Alhamisi, na juzi Jumapili ndio ilikuwa mara yake ya kwanza kuwa kwenye benchi la timu hiyo.

Akizungumza baada ya mchezo huo, Rangnick alimsifia Fred kwa uwezo wake na kuwezesha ushindi huo wa kwanza kwake.

Rangnick alisema: "Nafikiri kila mmoja anampenda Fred. Unatakiwa kumpenda Fred. Nimemjua yeye kwa siku mbili tu, lakini sasa anang'ara."

"Alionyesha kiwango bora na kwa hakika kabisa tulistahili ushindi ule, ingawa tulipaswa tupate mabao mengi zaidi."

# Ibrahimovic: Nataka kubaki Milan maisha

**MILAN, Italia**

ZLATAN Ibrahimovic anataka kubaki Milan kwa "maisha" wakati nyota huyo akiangalia uwezekano wa kuongeza mkataba na 'Rossoneri' hao.

Ibrahimovic alisherehekea kutimiza umri wa miaka 40 Oktoba mwaka huu, lakini mshambuliaji huyo hajaonyesha nia ya kupunguza kasi wakati Milan ikiwa kwenye windo la taji la Serie A.

Mkataba wake ukiwa unamalizika mwishoni mwa msimu huu, Ibrahimovic amefunga mabao sita katika mechi tisa za Ligi Kuu msimu huu.

Ibrahimovic ameonyesha kuimarika zaidi kwa kiwango chake tangu alipojiunga na Milan kwa kipindi cha pili Januari 2020 na raia huyo wa Sweden ameonyesha hana nia ya kuondoka pale San Siro.

"Nataka kucheza kwa muda mrefu kadri inavyowezekana," alisema Ibrahimovic - ambaye alikuwa sehemu ya timu ya Milan iliyoshinda kwa mara ya mwisho taji la Serie A msimu wa 2010-11 - akiiambia Rai.

"Hebu tuweke presha hapa kwa Milan kunipa mkataba mpya na nina matumaini ya kubaki Milan kwa maisha.

"Bado nina malengo ambayo natakiwa kuyapata na nataka kushinda tena Scudetto."



HABARI MICHEZO


,374,640

JACKPOT

MECHI WIKI HII

BASHIRI KWA USAHIHI MECHI ZOTE 13

| TAREHE | MUDA | MICHEZO | NYUMBANI 1 | SARE X | UGENINI 2 |
|---|---|---|---|---|---|
| 01. 11/12/21 | 18:00 | Peterborough vs Millwall | 3.04 | 3.19 | 2.29 |
| 02. 11/12/21 | 18:00 | Derby vs Blackpool | 2.34 | 3.14 | 2.99 |
| 03. 11/12/21 | 18:15 | Alaves vs Getafe | 2.37 | 2.94 | 3.34 |
| 04. 11/12/21 | 23:00 | Athletic Bilbao vs Sevilla FC | 2.64 | 3.09 | 2.79 |
| 05. 12/12/21 | 14:30 | Torino vs Bologna | 2.30 | 3.25 | 3.15 |
| 06. 12/12/21 | 15:00 | Lille vs Lyon | 2.50 | 3.49 | 2.65 |
| 07. 12/12/21 | 17:00 | Brighton vs Tottenham | 3.00 | 3.20 | 2.42 |
| 08. 12/12/21 | 17:00 | Metz vs Lorient | 2.35 | 3.28 | 2.99 |
| 09. 12/12/21 | 19:00 | Strasbourg vs Marseille | 2.64 | 3.34 | 2.59 |
| 10. 12/12/21 | 19:30 | Crystal Palace vs Everton | 2.27 | 3.20 | 3.25 |
| 11. 12/12/21 | 20:00 | Sassuolo vs Lazio | 2.89 | 3.49 | 2.34 |
| 12. 12/12/21 | 20:15 | Alcorcon vs FC Cartagena | 2.94 | 2.94 | 2.50 |
| 13. 12/12/21 | 20:30 | Betis vs Real Sociedad | 2.35 | 3.25 | 3.05 |

MECHI ZA USHINDI

"1" NI TIMU YA NYUMBANI KUSHINDA "X" NI TIMU KUTOKA SARE "2" NI TIMU YA UGENINI KUSHINDA.

JUMANNE - 07 - DESEMBA 2021

| TAREHE | GAMEID | MICHEZO | NYUMBANI 1 | SARE X | UGENINI 2 |
|---|---|---|---|---|---|
| 16:00 | 5943 | FK Vozdovac vs Vojvodina | 2.70 | 3.35 | 2.55 |
| 17:00 | 4812 | ASK Bravo vs NK Radomlje | 1.79 | 3.56 | 3.85 |
| 17:00 | 4858 | East Bengal vs FC Goa | 3.09 | 3.43 | 2.07 |
| 18:00 | 2604 | Jordan vs Palestine | 1.93 | 3.15 | 4.40 |
| 18:30 | 2068 | TS Galaxy FC vs Chippa Utd | 2.35 | 2.90 | 3.24 |
| 20:30 | 1276 | Cape Town City vs Maritzburg Utd | 2.37 | 2.56 | 3.74 |
| 20:45 | 1859 | RB Leipzig vs Manchester City | 3.24 | 3.77 | 2.06 |
| 20:45 | 4517 | Paris St Germain vs Brugge | 1.36 | 5.34 | 7.19 |
| 22:00 | 1459 | Lebanon vs Sudan | 2.10 | 3.10 | 3.85 |
| 22:00 | 4102 | Algeria vs Egypt | 2.50 | 3.00 | 3.05 |
| 22:45 | 1012 | Exeter vs Northampton | 2.06 | 3.34 | 3.39 |
| 22:45 | 1061 | Fleetwood Town vs Bolton | 3.03 | 3.38 | 2.20 |
| 22:45 | 1151 | Leyton Orient vs Swindon Town | 2.20 | 3.32 | 3.08 |
| 22:45 | 2005 | Enfield Town vs Bowers Pitsea | 1.44 | 4.42 | 5.57 |
| 22:45 | 2033 | Oldham vs Tranmere | 2.75 | 3.28 | 2.43 |
| 22:45 | 2157 | Nuneaton vs St Ives Town | 2.12 | 4.10 | 2.90 |
| 22:45 | 2187 | Accrington vs AFC Wimbledon | 2.46 | 3.35 | 2.66 |
| 22:45 | 2222 | Ebbsfleet vs Bath City | 1.29 | 5.03 | 8.12 |
| 22:45 | 2271 | Gateshead vs York City | 1.90 | 3.56 | 3.42 |
| 22:45 | 2535 | Folkestone Invicta vs Bishop Stortford | 2.18 | 3.61 | 2.75 |
| 22:45 | 2734 | Charlton vs Ipswich | 2.55 | 3.29 | 2.60 |
| 22:45 | 2768 | Wycombe vs Burton | 1.87 | 3.49 | 3.88 |
| 22:45 | 2944 | Sunderland vs Morecambe | 1.45 | 4.41 | 6.08 |
| 22:45 | 2968 | Portsmouth vs Sheffield Wed | 2.29 | 3.29 | 2.94 |
| 22:45 | 3019 | Walsall vs Crawley Town | 2.04 | 3.39 | 3.39 |
| 22:45 | 3030 | Harrogate vs Forest Green | 2.80 | 3.34 | 2.37 |
| 22:45 | 3364 | Mansfield vs Carlisle | 1.93 | 3.39 | 3.73 |
| 22:45 | 3403 | Crewe vs Lincoln | 2.98 | 3.33 | 2.25 |
| 22:45 | 3559 | Taunton Town vs Yate Town | 2.16 | 3.90 | 2.95 |
| 22:45 | 3720 | Newport vs Sutton United | 2.21 | 3.34 | 3.05 |
| 22:45 | 3761 | Haringey Borough vs Worthing | 5.03 | 4.54 | 1.47 |
| 22:45 | 3970 | Truro City vs Tiverton Town | 2.19 | 3.51 | 2.79 |
| 22:45 | 3995 | Rotherham vs Gillingham | 1.35 | 4.73 | 7.88 |
| 22:45 | 4233 | Alvechurch vs Tamworth | 2.27 | 3.53 | 2.66 |
| 22:45 | 4301 | Cheltenham vs Cambridge Utd | 1.90 | 3.53 | 3.68 |
| 22:45 | 4382 | Southend vs Maidenhead U | 1.88 | 3.57 | 3.67 |
| 22:45 | 4470 | Stevenage vs Scunthorpe | 1.87 | 3.44 | 3.93 |
| 22:45 | 4613 | Queen of South vs Cove Rangers | 2.36 | 3.42 | 2.60 |
| 22:45 | 4773 | Buxton FC vs Scarborough Athletic | 1.47 | 4.15 | 5.60 |
| 22:45 | 5001 | Morton vs Inverness | 3.35 | 3.35 | 2.15 |
| 22:45 | 5520 | Banbury United vs Biggleswade Town | 1.48 | 4.43 | 5.01 |
| 22:45 | 5617 | Guiseley vs Southport | 2.27 | 3.41 | 2.74 |
| 22:45 | 5684 | Bristol Rovers vs Port Vale | 2.65 | 3.29 | 2.51 |
| 22:45 | 5977 | Doncaster vs Oxford Utd | 3.73 | 3.43 | 1.92 |
| 23:00 | 1047 | Shakhtar Donetsk vs Sheriff Tiraspol | 1.53 | 4.40 | 5.60 |
| 23:00 | 1627 | Ajax vs Sporting Lisbon | 1.49 | 4.60 | 5.80 |
| 23:00 | 2127 | Porto vs Atletico Madrid | 2.75 | 3.20 | 2.60 |
| 23:00 | 3593 | AC Milan vs Liverpool | 2.14 | 3.59 | 3.19 |
| 23:00 | 4485 | Borussia Dortmund vs Besiktas | 1.27 | 6.21 | 8.82 |
| 23:00 | 4747 | Real Madrid vs Inter | 2.17 | 3.39 | 3.29 |

CHEZA KWA WAJIBU. KIWANGO CHA MAKATO YA SIMU KUZINGATIWA.


# WAZIRI BASHUNGWA AWAGEUKIA WAAMUZI 'WACHAFUZI' LIGI KUU

**Na Abdallah Khamis, MTWARA**



WAZIRI wa Utamaduni, Sanaa na Michezo, Innocent Bashungwa, amelitaka Shirikisho la Soka nchini (TFF), kutowafumbia macho baadhi ya waamuzi wanaotaka kudhoofisha mchezo wa soka nchini kwa kuhujumu baadhi ya timu kwa maslahi binafsi.

Aidha, Bashungwa amesema kwa sasa Ligi Kuu ya soka nchini inaenda vizuri na usimamizi wake unairidhisha serikali, hivyo wanapotokea baadhi ya waamuzi wanaotaka kuhujumu hali hiyo, ni vema vyama husika vikachukua hatua kwa wakati kwa ajili ya maslahi mapana ya mpira wa miguu nchini.

Basungwa alitoa kauli hiyo mkoani Mtwara juzi, wakati akifunga mashindano ya Umoja wa Michezo na Sanaa kwa Vyuo vya Ualimu Tanzania (UMISAVUTA), yaliyomalizika kwa Kanda ya Ziwa kuibuka mshindi wa jumla wa michezo yote huku kwa upande wa soka Kanda ya Mashariki ikiibuka mabingwa.

"Kuna mambo ya ovyo naamini wote tunaofuatilia soka tunaliona, waamuzi wachache wanataka kuharibu mchezo wa soka. Baadhi ya mambo wanayoyafanya yanawaumiza wengi, ni muhimu waamuzi wa aina hii wakachukuliwa hatua ili tusizikatishe tamaa baadhi ya klabu za soka kwani mazingira wanayotumia mpaka kufika katika kituo cha kuchezea ni gharama sana,"alisema Bashungwa.

Aliongeza kuwa ni vema sheria, taratibu na kanuni zinazowadhibiti waamuzi wasiotekeleza majukumu yao kwa ufanisi, zikatumika kwa ajili ya kurudisha imani kwa wadau wa mchezo wa soka nchini.

Kuhusu michezo ya UMISAVUTA, Waziri Bashungwa alisema kwenye mkakati wa serikali wa kuendeleza michezo nchini, ni pamoja na kutambua vipaji mbalimbali vinavyojitokeza maeneo tofauti ikiwa ni pamoja na kuwaandaa walimu wa michezo.

Alisema Wizara ya Utamaduni Sanaa na Michezo, itashirikiana kwa karibu na Wizara ya Elimu Sayansi na Teknolojia, pamoja na Ofisi ya Rais TAMISEMI, kuhakikisha mahitaji ya walimu wa michezo shuleni yanaendana na uzalishaji wa walimu hao katika vyuo vya ualimu.

"Nimefurahi kuona walimu wa vyuo vya ualimu nchini wana umoja wao na nimemwambia katibu mkuu wizara ya elimu tukutane na hawa wadau kwa ajili ya kupanga mkakati mzuri zaidi wa kuendeleza michezo shuleni huku tukiwapa kipaumbele walimu wa michezo,"alisema Bashungwa.

Mkuu wa Mkoa wa Mtwara, Brigedia Jenerali Marco Gaguti, alitumia nafasi hiyo ya ufungaji wa michezo ya UMISAVUTA kueleza kuwa michezo hiyo imefanyika kwa umahiri mkubwa na kuomba fursa zaidi za kimichezo zielekezwe katika mkoa huo.

Mwenyekiti wa Wakuu wa Vyuo vya Ualimu nchini, Doroth Mhaiki, ambaye ndiye mwenyekiti wa mashindano hayo ya UMISAVUTA 2021, alisema licha ya michuano hiyo kutokufanyika msimu wa 2020, kutokana na kuibuka kwa ugonjwa wa COVID-19, msimu huu wamefanya vizuri kuanzia maandalizi

# Mtibwa yaivutia kasi Biashara

**Na Dennis Fussi**

TIMU ya Mtibwa Sugar ina nafasi ya kurekebisha makosa yake ili iweze kupata ushindi wa kwanza wa Ligi Kuu Tanzania bara msimu huu, wakati itakapoikabili Biashara United, keshokutwa Alhamisi, kwa mujibu wa Ofisa Habari wa klabu hiyo, Thobias Kifaru.

Mtibwa itaingia kwenye mchezo huo ikiwa inaburuza mkia kwenye msimamo wa Ligi Kuu kwa kujikusanyia pointi mbili tu katika mechi saba ilizocheza hadi sasa, huku Biashara ikiwa nafasi ya 11 ikiwa na pointi nane.

Kifaru ameweka wazi kwamba, katika mchezo huo watapambana kila wawezavyo ili kuhakikisha wanapata ushindi na pointi zote tatu.

"Kiukweli timu yetu ipo kwenye wakati mgumu, lakini naamini hiki ni kipindi cha mpito tu, kwani mchezo wetu ujao lazima tupambane kuhakikisha tunapata ushindi," alisema Kifaru.

Mtibwa ambayo inanolewa na kocha Mcameroon Joseph Omog, imekuwa na matokeo yasiyoridhisha tangu kuanza kwa msimu huu mpya wa Ligi Kuu na ipo kwenye hatari ya kushuka daraja kama itaendelea kuwa kwenye kiwango hicho cha sasa.



# Michezo

Jumanne Desemba 7, 2021
Nipashe



Rangnick ampigia saluti Fred

MAANDALIZI...



Mshambuliaji wa Yanga, Fiston Mayele, akiwania mpira dhidi ya beki wa pembeni wa timu hiyo, Adeyum Saleh (chini), wakati wa mazoezi ya kujiandaa na mechi za Ligi Kuu ikiwamo ya Jumapili ijayo dhidi ya watani wao wa jadi, Simba itakayopigwa Uwanja wa Benjamin Mkapa. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

## Mayele: Tulieni tu, nitaifunga Simba

**Na Dennis Fussi**

NYOTA wa Yanga, Fiston Mayele amebainisha atahakikisha anaendeleza furaha ya mashabiki wao kwa kuifunga tena Simba watakapokutana Jumapili wiki hii katika mchezo wa Ligi Kuu utakaopigwa Uwanja wa Benjamin Mkapa, Dar es Salaam.

Mchezo huo utakuwa wa kwanza kwenye Ligi Kuu kuzikutanisha Simba na Yanga msimu huu, baada ya awali kukutana katika mechi ya Ngao ya Jamii na Mayele kuiua Simba kwa kuifungia timu yake bao pekee wakati wakishinda 1-0.

Akizungumza jijini Dar es Salaam, Mayele amesema anajua utakuwa mchezo mgumu kwake kwa kuwa mabeki wengi wa Simba watamkamia, lakini atapambana kuhakikisha anatimiza wajibu wake.

Alisema ana matumaini Yanga wanaweza kupata matokeo mazuri kwenye mchezo huo, ili kujiweka kwenye mazingira mazuri ya kuwania ubingwa wa Ligi Kuu.

"Simba ni timu nzuri, ina wachezaji wazuri wenye majina, lakini mimi na wenzangu tumejipanga kuwafunga tena," alisema Mayele ambaye hadi sasa ana mabao matatu kwenye Ligi Kuu.

# SIMBA YAANZA KAZI MBIO MAKUNDI CAF

### ●●● Yashusha kocha mpya wa makipa, majembe mengine yaja, yazikwepa Pyramids, TP Mazembe na RS Berkane katika droo...

**Na Waandishi Wetu**

IKIWA ni siku moja baada ya Klabu ya Simba kusema kwamba inakwenda sokoni kusajili wachezaji ambao watakiongezea nguvu kikosi chao kwenye hatua ya makundi ya michuano ya Kombe la Shirikisho Afrika, tayari imeanza kazi kwa kuimarisha benchi la ufundi upande wa kocha wa makipa.

Mwenyekiti wa Bodi ya Wakurugenzi wa klabu hiyo, Salim Abdallah 'Try Again', juzi alitoa kauli hiyo baada ya kumalizika kwa mechi ya mkondo wa pili ya mtoano katika Uwanja wa Mashujaa, Lusaka, Zambia dhidi ya Red Arrows ya nchini humo na Simba kufuzu hatua ya makundi.

Alisema wataongeza wachezaji kwenye uwezo wa kupambana kuhakikisha wanachukua ubingwa huo, hivyo kuwataka wanachama na mashabiki wa Simba watulie kwani mambo mazuri yanakuja na nia yao kwanza walihitaji kufuzu.

"Lengo ilikuwa ni kufuzu na tumefanya hivyo, tunashukuru pia mbinu za mwalimu, hasa mabadiliko aliyoyafanya ambayo yalisaidia sana pale tulipokuwa tuko nyuma kwa mabao mawili. Sasa gari limewaka na dirisha dogo tunakwenda kufanya usajili wa wachezaji kwa ajili ya kuchukua ubingwa huu, tunakwenda kufanya marekebisho kuhakikisha kuwa tunasajili, yaani kupata wachezaji ambao wanaweza kupambana na kuhakikisha wanachukua kombe hili," alisema mwenyekiti huyo.

Kocha Mkuu wa timu hiyo, Pablo Franco, mbali na kuwashukuru mashabiki waliungana na timu Zambia kuipa sapoti, alisema alikwenda nchini humo kushinda mechi, lakini hakufanikiwa kushinda, lakini anafurahi kuwa amefuzu.

"Nina furaha tumefuzu kwenye makundi, lakini haikuwa mechi rahisi kwani kipindi cha kwanza tulijitahidi kuwazuia wapinzani wetu na kuutuliza mchezo, tukakosa mabao mawili ambayo Hassan Dilunga aliyatengeneza kutoka pande zote mbili, kulia na kushoto, lakini baadaye tukapoteza umiliki, tukaruhusu bao," alisema kocha huyo.

Akisifia kikosi cha Red Arrows kuwa kuna wachezaji wazuri na wenye vipaji na kasi kubwa, hivyo amewapongeza wachezaji wake kuwa ilibidi wapambane sana ili kuwazuia.

Nahodha John Bocco yeye aliwashukuru wanachama na mashabiki waliotoka nchini Tanzania kwenda Zambia kuwapa sapoti, pamoja na Watanzania waishio nchini humo ambao walikuwa msaada mkubwa kwao kuwashangilia.

Naye Ofisa Mtendaji Mkuu, Barbara Gonzalez, alisema pamoja na kwamba timu haikucheza kwenye kiwango ambacho walitegemea, lakini wanafurahi kuwa wamefuzu kwenda hatua ya makundi.

"Pale ambapo tumekosea inabidi tujirekebishe, dirisha dogo linafunguliwa ni lazima tuangalie hali ya timu, kama tunahitaji kusajili basi tutaangalia tusajili maeneo gani yenye mapungufu," alisema Barbara.

Barbara alisema wanasubiri ripoti ya kocha wao Pabro Franco kuona wanaongeza nguvu kwenye maeneo gani ndani ya kikosi cha timu hiyo.

Simba ambayo imetinga hatua ya makundi baada ya kuiondosha Red Arrows kwa jumla ya mabao 4-2, baada ya ushindi wa mabao 3-0 nchini Tanzania, Novemba 28, mwaka huu, tayari Shirikisho la Soka Afrika (CAF), limeipanga katika 'chungu' kimoja na Pyramids ya Misri, TP Mazembe (DR Congo), na RS Berkane (Morocco) anayoicheza kiungo wao wa zamani, Clautos Chama. Hivyo timu hizo haziwezi kukutana katika hatua ya makundi.

Katika hatua nyingine, jana kocha wa makipa alitua rasmi nchini jana akitokea Afrika Kusini na anatarajiwa kuanza kazi Simba moja kwa moja wakati timu itakaporejea leo kutokea Zambia tayari kwa maandalizi ya mechi ya watani wajadi, dhidi ya Yanga, Jumapili wiki hii.

***Imeandaliwa na Saada Akida, Adam Fungamwango na Faustine Feliciane***

GAZETI HILI HUTOLEWA NA KUCHAPISHWA NA THE GUARDIAN LIMITED, S.L.P 31042

9 770856 541002 >